# Yehova-yire #3

Grass Valley, California, Amerika
Julai 07, 1962

1 Asante, Ndugu Borders. Mnaweza kuketi. Kuwa tu na ushirika fulani na Ndugu Harrel, mwenyekiti wa mkutano, na kuona yeye amekuwa mmishenari, na sisi ni namna ya kuwa na mambo yanayofanana. Yeye anarejea sasa katika Pwani ya Dhahabu, Afrika. Na mimi ninalenga kuwa kule mwaka huu. Tulikuwa tunajaribu kuweka jambo fulani pamoja juu ya kutembelea Pwani ya Dhahabu baada ya kuja kutoka Afrika Kusini.

Hivyo tulikuwa, kile ninachofikiri, mmojawapo wa mikutano mikuu, katika siku yangu, ulikuwa katika Afrika Kusini, tulipoona umati wa wenyeji elfu thelathini waliovaa mablanketi wakimpokea Kristo kwa wakati mmoja. Amina. Wao waliwaomba wavunjevunje sanamu zao ardhini, kuwa kwa kweli wao walimaanisha hilo. Nao walivunjavunja sanamu zao, kama tufani ya vumbi ikija, na kumkubali Kristo kama Mwokozi wao, kwenye mkutano mmoja. Wao walikuwa na ufuatiliaji mzuri kule, hivyo wao-wao waliwapata.

2 Lakini ule wito mkuu zaidi wa kuja madhabahuni ninaoweza kukumbuka, wa Bwana akitupa sisi, ulikuwa katika...ulikuwa kule India, pale ambapo tulikuwa na kama elfu mia tano katika mkutano mmoja. Na kule sisi-sisi hatukuweza tu kukadiria; ni umbali tu ambao uliweza kuona, ilikuwa tu kila mahali. Na wote walimkubali Kristo kama Mwokozi wao, lakini pasipo na kitu kimoja cha kufuatilia nacho. Hivyo basi, bila shaka, Shiite, waliwachukua walio wao, Jains wakawachukua wa kwao, na kadhalika. Nadhani wengi wao walirejea, ili kuona jambo fulani Bwana analofanya na kupatikana kule.

Ile huduma yangu Bwana aliyonipa, katika Amerika haina nguvu sana, ni watu wa Pentekoste tu. Mengi ya makanisa ya Kiamerika ni makanisa yenye kutumia akili zaidi, nayo yanaamini kanuni ya imani ya dini. Na hapo ndipo tu wanapokaa, huwezi kuwaondoa kutoka kwenye hilo.

Lakini unapomchukua mzawa mwenyeji na kujaribu kumwambia jambo fulani juu ya kanuni ya imani ya dini, yeye hata hajui upi ni mkono wa kuume na wa kushoto. Hilo lina faida gani kumpa yeye kitini? Inabidi yeye aone jambo fulani. Na yeye anapoona hilo, ndipo yeye anashawishika. Na anamwona mchawi wake akiinuka na kulipinga hilo, na kumwona Roho Mtakatifu akiliangusha hilo pale pale. Naam. Basi hilo-hilo linaonyesha hilo, Mungu ni Nani, na ndipo hilo linakuwa limekwisha.

3 Na hivyo tulipoonana na Ndugu Harrel tulifurahi sana! Nilikuwa ninazungumza tu juu ya wale wenyeji wa Afrika. Yeye alikuwa anazungumza juuu ya kudhamini mmoja wa Ndugu T.L. Osborn.

Wengi wenu mnamjua Ndugu Osborn, nadhani. Ee, kuna mtumishi wa thamani wa Kristo, Ndugu Osborn. Yeye ni mmojawapo wa marafiki zangu wa ndani ya moyo. Kwa kweli ninayo heshima ya kilindi katika moyo wangu kwa ajili ya Ndugu Osborn, mmishenari mkuu kama huyu. Naamini-naamini yeye amefanya mengi zaidi kwenye mashamba ya huduma ya misheni kuliko mtu mwingine yeyote duniani leo, yule ninayemfahamu, ni-ni Ndugu Osborn. Mvulana mpenzi, mzuri, na hakika nampenda Ndugu na Dada Osborn.

4 Wao wananiambia kuwa Mama Arganbright yuko mkutanoni jioni hii. Je, unajificha nisikuone, Mama Arganbright? Kwa kweli nashukuru kwa tunda lako zuri. Na si ajabu yeye ni bibiye mzuri sana, yeye anatokea sehemu hii ya nchi hapa. Yeye siku zote anazungumza juu ya Grass Valley. Ni wangapi wanawafahamu Bw. Na Bibi Arganbright, kule Grass Valley? Vema, hilo ni jema. Uko wapi, Mama Arganbright? Sijakuona kwa muda mrefu, ulichopoka ...Yule pale. Ndiyo. Bariki moyo wake. Nyumbani kwake ni nyumbani kwangu kwa pili, mwanamke wa ajabu kutokea hapa hapa Grass Valley. Na siku zote yeye amekuwa na mzigo kwa ajili ya hawa watu. Na ndugu Arganbright, kama hii ni ibada ya jioni ya kwanza hapa, nilikuwa kule nje msituni nikiiomba leo wewe mlipomtembelea mke na hao. Na samahani sikuwepo ili nikuone, na wewe ukutane na rafiki yako.

5 Lakini nitasema kuwa nimeona jambo fulani likitukia miongoni mwa watu wako hapa ambalo sijawahi kuona katika jiji lingine la Amerika kokote. Nimewaona Wakristo wakitambua kuwa wao wamekosea, kwenye Neno la Mungu, na kusimama na kuomba

rehema. Naam. Hilo linaonekana kwangu kama uamsho ungeweza kulipuka ndani hapa. Hilo lingekuwa zuri mno. Kwa kiasi nilichohubiri ulimwenguni, na hasa katika Amerika, kamwe sikuwahi kuona hapo kabla, makundi ya Wakristo, neno lilipoletwa chini ili kulionyesha Neno, wao wanainuka na kusema (nilishuhudia) walikuwa wamekosea. Siyo hilo tu, wahudumu pamoja nao. Sasa, huo ni uaminifu. Nalipenda hilo.

Dada Arganbright, Ben alikufanya usimame wima.

6 Nakwenda kumfedhehesha mke wangu. Yeye ni mtu mwoga kuliko wote ulimwenguni. Lakini yeye ameketi hapa jioni hii. Mpenzi, naamini utanivumilia kwa hili, lakini nitamuomba mke wangu asimame wima. Mwanamke mzuri zaidi ya wote katika ulimwengu wote, kwangu. [Kusanyiko linashangilia-Mh.]

Msichana wangu, binti yangu, binti yangu mkubwa zaidi ya wote, Rebeka. Sasa, mpenzi, najua umeunguzwa na jua, lakini nataka usimame wima, hata hivyo. Vema, Rebeka. Huyo ni binti yangu, Rebeka. [Kusanyiko linashangilia-Mh.] Asanteni. Asanteni.

Ndugu Jewel Rose, ni wangapi wanaomfahamu? Jioni moja alimfanya mke wangu aje jukwaani nilikokuwa, baada ya hiyo kuwa imekiwshakuanza. Na mke wangu alikaribia kuzimia. Mke wangu huwa anamkwepa tu kila mahali anapomwona yeye. Yeye anaondoka njiani mwake, kwa sababu anaogopa yeye atamwita aje jukwaani tena.

Nilimwambia, "Jioni moja nakwenda kukuinua na unene kwa kitambo kidogo kwa ajili yetu."

Yeye akasema, "Andaa ndoo ya maji, kwa sababu nakwenda kuzimia."

Yeye ni mtu wa mpendwa sana, mke wangu. Kama kuna sifa yoyote ya kupewa familia ya Branham, hebu iende kwake. Yeye ndiye aliyesimama kati yangu na hadhara ya watu. Na mambo yote yaliyofanyika kwa usahihi, ndiye yeye amefanya hilo.

7 Natumaini kuwa kila mwanamume kijana hapa, yeye atakapooa, atapata mke, na mtaishi kwa furaha pamoja kama mke na ninayo hii miaka ishirini na mbili ambayo tumeoana.

"Yeye ampataye mke, amepata kitu chema." Kama Sulemani alivyosema, "Mwanamke mwema ni kito cha thamani katika taji ya mwanamume. Aliye mwovu ni maji katika damu yake." Na mkondo wa damu yake ni uzima wake. Hivyo, yule aliye mwovu ni kitu kibaya zaidi anachoweza kukishikilia. Na yule mwenye haki ni kitu kilicho bora zaidi yeye anachoweza kukishikilia, nje ya wokovu. Kama Mungu angeliweza kumpa mwanamume kitu kilicho bora kuliko mke, Yeye angelimpa yeye hicho, kwa sababu Mungu huwapa tu watoto Wake vitu vizuri. Na Yeye alimpa mke, nami nashukuru kwa hilo.

Na kuwaona wanawake, wakati mimi namna ya kuumiza jioni ile nyingine. Kwa Andiko kwa namna ambayo hawa wanawake wa Pentekoste wanavaa, wanavyovaa nywele zao, na kuendelea. Unasema, "Hilo halileti tofauti yoyote." Hakika linaleta tofauti.

8 Nataka kuwauliza jambo fulani. Ndugu Harrel hapa, mmishenari.

Kule Durban, Afrika Kusini, wanawake walikuwa wameketi kule wakiwa uchi kama walivyokuja duniani; kamwe hawakuwahi kuwa na kipande kimoja cha nguo, kishada tu kidogo, kama inchi nne, sita kikiwekwa mbele yao. Na wakiwa wamesimama pale uchi kama walivyokuwa, nao wakiwa wamesimama ardhini baada ya huu muujiza mkuu wa kimiujiza kutokea jukwaani. Na kulikuweko katika lile kundi, karibia Waislamu elfu kumi (kwa wakati mmoja) waliomkubali Kristo katika mkutano huo huo. Na ndipo ndani pale wakati...Hawa wanawake, wakiwa wamesimama pamoja na hawa wanaume, walimkubali Kristo.

Na Ndugu Bosworth alisema, "Ndugu Branham, naamini wewe unapaswa kupiga simu tena. Naamini wao wanamaanisha uponyaji wa 'kimwili'"

9 Na nilisema, bila shaka, mbele ya wafasiri kumi na tano mbalimbali. Unajua hilo linahitaji...Inakupasa uandike kile ulichosema, wakati wao...Unasema, "Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, alikuja kuwaokoa wenye dhambi." Na huyu atakwenda "blu, blu, blu, blu," na huyu mwingine "niki, niki, niki, niki," huyo ni "Yesu Kristo, Mwana wa Mungu."

Unajua, mimi-mimi nilikuwa nikisikia watu wakinena kwa lugha, na nikawaza, "Jamani, hilo haliwezi kuwa sawa." Lakini Biblia ilisema, "Hakuna sauti isiyokuwa na

maana." Hakuna. Niliposikia hilo, baadhi yao wakitoa sauti kama kuku kuita vifaranga, baadhi wakitoa sauti kama ya ndege, na kila kitu. Lakini hilo linamaanisha maana fulani kwao, kama kila sauti ilikuwa na maana.

10 Na ilipokuja tena, nikasema, "Vema, basi hao wajue ambao wanajua hasa hilo siyo uponyaji wa kimwili, ni kumpokea Kristo kama Mwokozi, mbingu ya kwenda, unaamini katika Mwana wa Mungu, unamkubali Yeye kama Mwokozi wako kibinafsi, unavunja vinyago vyako ardhibi." Nao wakavitupa chini, Nami nikasema, "Sawa pale sasa, inueni mikono yenu kwa huyo Mungu na kumsifu Yeye. Atawapa Roho Mtakatifu."

Na walipokuwa wamesimama kwenye hiyo ardhi, niliwaona wanawake waliokuwa uchi wa mnyama; na mara baada ya Kristo kuwagonga, waliondoka kutoka kwenye huo uwanja wakiwa wamekunja mikono yao. Na unapowaona tena, walikuwa wamevaa nguo.

Sasa, kama Kristo atamfanya kafiri (aliye uchi) atambue kuwa yeye ana makosa kuwa uchi, na ndipo hao wanawake wanaokiri kuwa Wakristo na kila mwaka wakivua nguo zaidi, mimi siwezi kuelewa hilo. Kuna kitu fulani cha makosa mahali fulani.

Kafiri mjinga, akiwa amesimama pale, aliyezaliwa katika ulimwengu huu na kamwe hakujua yeye alikuwa uchi, yeye hajui yuko uchi. Lakini hebu Kristo aje katika uwepo wake, yeye anatambua yuko uchi, mno kiasi kwamba anajaribu kujifunika mwenyewe kadiri awezavyo, kukunja mikono yake na kuondoka. Siku mbili au tatu baadaye, utamkuta tena, yeye amevaa nguo.

Sasa kuna jambo fulani la makosa mahali fulani, na nina hakika siyo kwa Kristo. Ee, nafikiri Neno ni kamilifu!

11 Naipenda tu safari ya Abrahamu. Je, wewe huipendi? [Kusanyiko linasema, "Amina-Mh.] Ninakaa nayo kwa muda mrefu, natarajia kufikia Yehova-Yire jioni hii. Nilichukua somo langu nyakati tatu au nne za jioni zilizopita, na kamwe sikulifikia hilo.

Lakini mwaka mmoja kule nyumbani nililichukua somo, nikihubiri juu ya Ayubu. Vema, kwa karibu mwaka mmoja nilikuwa katika Kitabu cha Ayubu, kila Jumapili na Jumatano, juu ya Ayubu. Na hatimaye nilimpata hadi alipoketi juu ya lundo la majivu. Nilikuwa naye pale karibu wiki tatu au nne. Na dada mmoja wa thamani akiwa na ujasiri wa kutosha kuniandikia, yeye alisema, "Ndugu Branham, utakwenda kumwondoa Ayubu kwenye lundo la majivu?"

Vema, nadhani mnashangaa ni lini ninakwenda kumpata Abrahamu ili kumwona Yehova-Yire.

12 Lakini nilikuwa na jambo moja. Abrahamu ... Au, Ayubu akiwa ameketi pale kwenye lundo la majivu, Elihu akiwa ananena. Mungu akimjaribu mtakatifu. alilileta lote hadi hatimaye, hadi nifikie sehemu hii ambapo ningeweza kupiga risasi ya kuua, nilikuwa nimeandaa kila kitu. Ndipo Bwana akashuka chini katika huu upepo wa kisulisuli, radi zakaanza kumulika, na ngurumo zikanguruma. Na Roho wa Mungu akaja juu ya yule nabii, yeye akasimama kwa miguu yake, akasema, "Namjua Mkombozi wangu yu hai;" tazama "Mkombozi." "Na penye siku za mwisho Yeye atasimama juu ya nchi. Na hata kama hatimaye funza wa ngozi wanaharibu huu mwili, bado nitamwona Mungu katika mwili wangu; Huyu Ambaye nami nitamwona mimi nafsi yangu, macho yangu yatamtazama, na siyo mwingine." Ee, ni somo lililoje pale! Ili kuliingiza hilo ndani, inahitaji kitambo kidogo ili kufanya watu wote wakae vizuri, Roho kwa usahihi tu, ndipo ulilete hilo. Na ndipo madhabahu ikaitwa na kujazwa na watu, wanaoungama.

13 Kama tu wewe unaongozwa na Roho, chukua tu muda wako hadi uwe umelenga kwa usahihi. Kama hutafanya hivyo, utapiga risasi juu zaidi au upige risasi nje zaidi, au kitu fulani. Hebu tulenge kwa usahihi, Biblia! Naamini kwamba Mungu anataka sisi tulenge kwa usahihi. Roho Mtakatifu alilenga kwa usahihi pamoja na mitume, au wao walilenga kwa usahihi kwa Roho Mtakatifu, ndiyo namaanisha. Nami naamini sisi tunaweza kufanya jambo lile lile, kwa njia ya Neno lile lile. Hilo limepiga lengo! Na kama likipiga hilo wakati mmoja, pale pale katikati, linaweza kulipiga tena! Lakini yakupasa ulenge kwa usahihi! Uwe na hakika na kupumua kwako, kuvuta kwako, kila kitu ni sawa tu. Mimi huwa napiga risasi malengo, najua hicho ni kitu gani, unakaa katika kulingana vema, pamoja na bunduki itakayoweza kulenga kwa usahihi.

14 Wakati mmoja nilipeleka aina ndogo ya sabini na tano kwenye Kampuni ya Winchester, siku moja. Na sikuweza kuifanya hiyo ipige pale kama tatu…au robo inchi,

penye umbali wa yadi hamsini. Na Kampuni ya Winchester wakairudisha kwangu, walisema, "Mchungaji Branham, hiyo bunduki ilitengenezwa tu ku-kukusanya kundi la risasi tano, inchi moja penye umbali wa wa yadi ishirini na tano." Sasa hiyo ilikuwa kampuni iliyoitengeneza. Mimi najua tofauti. Nilikwenda tu, penye msitari, kwa usahihi, tisa moja kwa moja, misumari midogo ya zulia, penye umbali wa yadi hamsini, pamoja nayo. Hivyo nilijua ilikuwa imelenga kwa usahihi. Hivyo niliendelea kucheza nayo na kucheza nayo, hadi nikaipata ikirejea tena.

Sasa, kitu kile kile ni kwa njia ya Neno la Mungu.Hayo mambo hao mitume waliyofanya, haya mambo ambayo Kristo aliahidi, inatupasa tulenge kwa usahihi kwa Neno, kwa Roho. Kama hilo lilifanya hilo wakati mmoja, hilo litatenda tena, kwa sababu ni Mungu. Na Mungu ni Neno, na Yeye hawezi kushindwa.

15 Kama kusitisha kwa namna fulani, bunduki inaweza kuwa imelegea mno hapa katika kiganja cha mkono, kulegea kidogo au kukaza zaidi, chochote kile kinachoifunga hiyo, unaweza kuweka uzito wa kidole chako juu ya bunduki, na (ikapiga risasi kikamilifu) uzito wa kidole chako utaifanya ipige. Inakupasa uwe na kila kitu kikiwa kikamilifu.

Hivyo ndivyo inakupasa kufanya katika Ukristo, kulifanya Neno, kulifanya hilo lidhihirike na kutenda kwa usahihi, wewe mwenyewe pamoja na Neno na pamoja na Mungu, inapasa liwe kamilifu, na ndipo litalenga kwa usahihi. Inapasa iwe hivyo! Kwa hiyo basi, katika kuhubiri, unapaswa kumhisi Roho kwa usahihi tu, ndipo unapolenga kwa usahihi; hiyo itaondoka, itakwenda kwenye lengo.

16 Ndipo watu walioketi pale, mara nyingi watu husema, "Ndugu Branham, mimi sisikii juu ya mikutano yako."

Mimi sina njia za kutolea kama wanavyofanya hao ndugu wengine. Wao wana magazeti, wao wana-wao wana redio, televisheni. Mimi napita tu na kujaribu kumwakilisha Bwana Yesu. Watu wanaliona hilo, wanaliamini hilo, wanapona. Mungu anajua hilo, na hilo tu lililo la lazima. Unaona? Sisi hatu, siyo…Hapatakuweko na historia iliyoandikwa. Usijali kuhusu hilo. Hapatakuweko na wakati wa kuandika historia. Naamini Yesu anakuja. Hilo, mimi naamini hilo. Na nataka niishi leo kama Yeye angelikuja leo au kesho. Hakuna mashule makubwa makuu, na kadhalika. Tunafanya nini na hivyo vitu, na halafu tunahubiri Yesu anakuja? Mbona, matendo yetu wenyewe yanashuhudia dhidi yetu. Hilo ni sahihi. Yesu anakuja, hebu tuwe, tulifanye kanisa liwe tayari kwa ajili ya hilo! Hebu tuwe tayari. Ee, ninampenda Yeye iliyoje!

17 Hebu tuinamishe vichwa vyetu sasa kwa ajili ya neno la maombi. Ee, ninapenda iliyoje kuona watu wanainamisha vichwa vyao kwa unyenyekevu. Sasa hebu tukae tu kimya kwa kitambo kidogo, na tujifunze. Sasa tunataka kuchukua muda wetu. Kesho ni Jumapili, sabato, siku ya sabato ya Mkristo. Na sitaki mchelewe kwenye shule ya Jumapili, ijapokuwa hatutaki kuharakisha haya mambo.

Waza sasa, "Bwana, ni shauku yangu katika moyo wangu jioni hii kulingana na mapenzi Yako?" Kama ni hivyo, basi wazia hilo. Ndipo kama unaliwazia hilo, shauku yako, na kuichunguza hiyo kwa mpango wa Mungu. Kama inaonekana tu kuwa sahihi na mpango wa Mungu, basi nataka wewe umwinulie Mungu mkono wako juu, na useme, "Mungu, nikumbuke, hili ndilo ninalohitaji." Waza tu kwa bidii hasa. Mungu akubariki. Vizuri. Bwana akubariki. Hilo ni zuri. Endelea tu kuinua mkono wako juu. Yeye anaona yote, Yeye anajua mambo yote. Hilo ni zuri. Mungu akubariki. Amina. Mungu akubariki. Hilo ni zuri. Endelea tu kuwaza, ukiwa umeinua mkono wako juu. Sasa natazama kila mkono unapoinuliwa juu. Vema. Hilo ni jema.

18 Baba wa Mbinguni, tunakuja sasa, tunakaribia tena katika hilo Jina la Bwana Yesu linalotosheleza, hadi kwenye Kiti cha Rehema. Kama mtunga shairi alivyosema, "Hebu mimi kwenye Kiti cha Rehema, nipate kuwa huru kwa mapenzi." Mungu, mioyo yao imelemewa na kitu fulani. Na hebu wao sasa, penye Kiti cha Rehema, wapate faraja Mungu anayowaachia, yule Tabibu mkuu, na imani kwa ajili ya hicho wao walichohitaji.

Nimeinua juu mikono yangu yote miwili. Ninayo mahitaji. Nikumbuke, Bwana.

Wakumbuke watu hawa wote hapa wanaowakilishwa na hizi leso. Ee, jinsi shuhuda zilivyokuja ndani kwa sababu ya haya mambo. Unyenyekevu. Nje kule kuvuka hivi vilima vya mchanga hapa, mahali fulani, akina mama wagonjwa, akina baba, watoto wadogo, watu hospitalini, baba mzee aliye kipofu akiwa ameketi nyuma katik chumba kidogo

akiwa na bakora nyeupe mkononi mwake, akisubiri kurudi kwa hizi leso. Mungu, uturehemu. Tujalie, Bwana, kwamba yeyote zitakayewekwa juu yake, hebu yule adui aondoe uwezo wake na nguvu, hebu wao waende na kuponywa. Hapa kuna moja iliyoandikwa hapa, "saratani." Hebu hilo pepo liwaache huru, Bwana. Na hebu Roho Mtakatifu, Mungu anapotazama chini kupitia Damu ya Mwana Wake Mwenyewe aliyekufa kwa ajili ya hili kusudi, hebu ule upatanisho mkuu utosheleze jioni hii, na imani itiririke kwa wingi juu yao, na hebu…au kwa wingi, kwamba wao waweze kupokea uponyaji wao. Tujalie hilo, Bwana.

19 Bariki Neno Lako sasa. Msaidie mtumishi Wako, tupake mafuta kwa ajili ya huduma. Paka mafuta kila moyo unaosikia. Na tunakwenda tu kunena sasa, Baba. Utuambie kile cha kusema, na utuambie cha kufanya. Tunakutarajia Wewe uwe pamoja nasi katika mkutano.

Asante kwa ajili ya nyimbo nzuri jioni hii, hizo tenzi nzuri. Huyu mwanamume kijana nyuma hapa, Ndugu Heimer, aliimba tu huo utenzi mzuri, Yule Mgalilaya. Hebu huyo Mgeni Mgalilaya aingie ndani sasa jioni hii. Hebu sisi tusikie Sauti Yake ikiambia akili inayosumbuka, kama Yeye alivyofanya yale maji yanayosumbuka, "Amani, tulia." Na hebu kila moyo unaosumbuka uponywe. Tunaomba hilo katika Jina la Yesu. Amina.

20 *Ibrahimu akapaita mahali hapo Yehova-yire: kama ilivyoandikwa, Katika mlima wa Bwana itaonekana.*

Sasa tunataka kuanza na huyu mtu wa kipekee mkuu. Na kesho…Sasa, Bwana akipenda, tunakwenda kujaribu kufikia mwisho juu ya Abrahamu jioni hii. Na kesho somo juu ya uponyaji wa Kiungu.

Bwana amekuwa mwema kwetu hapa. Tumekuwa tukisikia shuhuda za yale mambo yaliyotukia. Na kufurahi mno! Na tulikuwa na ibada moja ya jioni, msitari kamili wa maombi, au kuwaita hao. Na hapakuwepo na mnyonge mmoja aliyeonekana ndani ya jengo, kiti chenye magurudumu, kokote, isipokuwa yule aliyeinuka, akitembea huku na huko, akitembea.

Na sasa kila jioni Roho Mtakatifu ameingia ndani katika utukufu Wake, Uwepo uliotukuka, na amekwenda kupitia kusanyiko, akijitangaza Mwenyewe, kwamba Yeye yupo hapa. Basi, tunapaswa kumwamini Yeye. Unaona, Yeye anataka wewe umwamini Yeye. Heshima ya hali ya juu zaidi iwezayo kumlipa Mungu ni kumwamini Yeye. Ni lazima uamini. "Yeye ajaye kwa Mungu lazima aamini kuwa Yeye Ndiye." Na sasa mwamini Yeye!

21 Na ninapomchukua Abrahamu, ile safari, ni kwa sababu tu ninajaribu kujenga imani kwa ajili ya mwisho mkuu, ili kuruhusu watu waweze kujua wao ni akina nani.

Hilo ndilo tatizo. Naona madaraja mawili ya watu, ninaposafiri. Mojawapo ni pentekoste, hilo lingine ni lile la washikilia imani kali ya kidini. Sasa, hao washikilia imani kali ya kidini wanajua pale walipo, kile wao walicho, lakini hawana imani yoyote na hilo. Pentekoste wana imani, lakini hawajui wao ni akina nani. Sasa, ni kama tu mtu aliye na fedha katika benki, lakini yeye hajui jinsi ya kuandika hundi; na yule mwingine anaweza kuandika hundi, na hana fedha katika benki. Kama ungewahi tu kuwaweka pamoja, kitu fulani kingetukia. Kama ungewahi kupata imani ya kipentekoste na fundisho la kushikilia imani kali ya dini, kama ungeweza… au ama uchukue fundisho la kushikilia imani kali ya kidini na imani ya kipentekoste, kitu fulani kinakwenda kutukia. Hilo ni sahihi.

22 51Sasa, ningependa iliyoje kutoa ushuhuda hapa, nilipoona, shule ya Lutheran, mia nne wakipokea Ubatizo wa Roho Mtakatifu nilipokuwa nikinena nao juu ya hilo. Lo, jamani, ulikuwa muonekano mtukufu, kuwaruhusu wao wajue hilo. Wao siyo, kwa sababu wao ni Walutheri, kuwa wao hawahesabiwi.

Hakuna chochote dhidi ya Baptisti, Methodisti, kwa kile wewe ulicho, Katoliki. Mimi siko kinyume na hayo mambo. Mimi siko kinyume na hao watu. Ni ule mfumo unaowashikilia ndio ninaonena dhidi yake. Hakuna chochote dhidi ya mtu binafsi, wote ni wanadamu ambao Kristo aliwafia; Mkatoliki, Myahudi, yeyote yule awaye. Ni huo mfumo. Kama Mwislamu, Shiite, Jain, au chochote kile, ni mfumo. Budha ni mfumo, unaona. Siyo hao watu wanaoabudu Budha; ni mfumo unaowavuta watoke.

Hicho ni kitu kile kile. Yesu hakuwa kinyume na watu. Yeye alikufa kwa ajili yao. Ilikuwa hiyo mifumo iliyokuwa inamzuia Yeye, ikiwaweka mbali na Yeye. Hicho ndicho kitu chenyewe hasa.

23 Sasa nilifikiri, katika kumchukua Abrahamu, tukijua kwamba ile ahadi alipewa Abrahamu, na Uzao wa Abrahamu baada ya yeye. Sasa hebu tusafiri nyuma kidogo na tupate msingi, na tuje jioni hii moja kwa moja kwenye somo lenyewe kwa kitambo kidogo.

Na kadi za maombi zitatolewa kwa mtu yeyote anayetaka kuombewa. Na sisi, kama hamtazipata wote jioni hii, tutazipata kesho. Na mtu yeyote anayetaka kuombewa lazima awe na kadi ya maombi. Na mmwe hapa penye saa saba na nusu kesho, ili kuchukua kadi yako ya maombi, kwa sababu tunataka kuanza mkutano wakati huo. Ndipo tutaomba kwa ajili ya kila mtu anayeshikilia kadi ya maombi kesho. Tumekuwa tukijaribu, kwenye nyakati za jioni, kuwafikia hao wasio na kadi za maombi, ili kwamba hao wenye kadi za maombi watakuwa na heshima ya kuwa katika msitari wa maombi. Na hao wengine wanaitwa huko, pasipo kuwa na kadi za maombi. Hilo linapata kuwili, pande mbili. Kadi ya maombi haimaanishi chochote. Lakini unampa mtu kadi ya maombi, na kuna kama asilimia arobaini wanaoponywa wakati huo huo, unawazia tu kuja kwenye msitari, kitu fulani unachoweza kushikilia, kitu fulani unachoweza kukitazama, au kitu fulani. Na huyo-huyo kijana atakuwa anatoa kadi za maombi kesho penye saa saba na nusu, ili wao waweze kuondoka penye saa nane, ili kwamba hayo mazoezi mengine ya siku waliyo nayo.

24 Na ninyi mnaotaka picha, kitabu, au kanda, lazima muwe navyo jioni hii. Hakuna kuuza Jumapili; kamwe haturuhusu hilo, kuviuza hivyo. Tunaiheshimu Jumapili, msiuze kabisa Jumapili. Na hivi vitabu na vitu, si kitu chochote kwangu, ni vitabu ambavyo watu wameandika juu ya huduma yangu. Picha ambazo American Photographer Association walipiga picha, na ni mali ya Douglas Studio, imemilikiwa. Hicho kitabu ni mali ya Ndugu Gordon Lindsay na Kasisi Julius Stadsklev. Tunavinunua na kuvileta kwenye mkutano, na kuviuza kwa kama kwa ile bei tunayonunulia, na hasara juu yake. Na siku zote tumesema hili, kama yeyote…Nimewaambia watu wanaouza vitabu, "Kama mwanamume au mwanamake anakuja juu hapa, mtu masikini, asiye na fedha ya kununua hicho kitabu; wapeni hicho, hata hivyo. Na sisi tuta…Nitahakikisha hilo linashughulikiwa." Na kama unacho kitabu na hakina thamani inachostahili, kirudishe. Hakuna kamwe kitakachorudishwa pasipo chochote bali kurejeshewa fedha yako, unaona. Ni kitu fulani tu cha kusaidia imani yako. Ni hilo tu tunalojaribu kufanya kwa hicho, vinginevyo tusingeruhusu hicho kiwe hapa. Hiyo ni sahihi kabisa. Hivyo sasa jioni hii, kumbukeni, vitakuwa kwenye sehemu ya kuweka vitabu. Rafiki yangu mwema, Bw. Na Bibi Wood. Natamani ningekuwa na muda niwaambie ushuhuda wao, wa jinsi mwana wao alivyoponywa polio. Na mambo mengine mengi yaliyotukia, ya watu walioko hapa katika mkutano.

25 Sasa hebu tuweke msingi wa Abrahamu. Kwanza, Mungu alikutana na Abrahamu, pasipo masharti, agano. Yeye alilofanya na Abrahamu. Siyo kitu chochote hata kidogo, Abrahamu hakuwa na chochote cha kufanya isipokuwa kumwamini Mungu. Lile agano kwa neema tu, na pasipo masharti. "Siyo, "kama utafanya". Mungu alisema, " Nimekwisha kufanya!" Na sasa kila mtu…

Kumbukeni, Uzao wote wa Abrahamu uliowahi kuja kwa Mungu, huja kwa njia hiyo hiyo. Hakuna chochote uliweza kufanya! Usingeweza kujiokoa mwenyewe zaidi kuliko ambavyo usingeweza kuchukua kamba za kiatu chako na kurukia mwezini. Huwezi kujiokoa mwenyewe. Hakuna mtu aliyewahi kumtafuta Mungu, ni Mungu anayemtafuta mtu. "Ninyi kamwe hamkunichagua Mimi," Yesu alisema, "Mimi niliwachagua ninyi." Mara ya kwanza…?...

26 Ungeweza kwenda nje hapa na umwambie nguruwe kuwa amekosea, kula mabaki ya vyakula mezani? Yeye atakuambia ushughulike na mambo yako. Lakini itahitaji jambo fulani ambalo lingeweza kubadilisha asili yake, ili kumfanya yeye atambue kuwa ana makosa. Inapasa jambo fulani litukie kwa huyo nguruwe, kwanza.

Hiyo ndiyo sababu hao wanaoitwa Wakristo mara nyingi hujiviringisha katika matope, kurudi kwenye dhambi, ni kwa sababu…Ungeweza kumsafisha nguruwe, na kupaka kucha zao rangi, na kupaka midomo rangi. Hilo, hilo ni kosa, lolote lile lililowahi kuwa. Poda nyekundu ya mdomo, sivyo, au jambo fulani? Napata hilo, jambo lote hilo, likiwa limechanganyikana. Mnajua ni kitu gani, hata hivyo. Unampaka nguruwe jike wa kale poda nyekundu mdomoni na-na, unajua, unamfanyia hayo matendo mengine, naye atakwenda moja kwa moja matopeni, na kugaagaa matopeni tena. Kwa nini? Yeye ni nguruwe jike, tangu mwanzo. Njia pekee ya kumfanyia yeye tofauti, ni kubadili asili

yake.

Hiyo ndiyo njia pekee ambayo mwanamume au mwanamke anaweza kumlingana Mungu, ni kubadili asili, kujisafisha, kufa kwa ile dhambi ya mtu wa kale, na kuzaliwa upya kwa njia ya Roho wa Mungu. Na, hiyo ni, Kristo ni Roho wa Mungu, na Kristo ni Neno. Basi hilo linashuhudia pamoja na Neno. Hiyo ndiyo njia pekee tutakayoweza kufanya hilo.

27 Sasa, Abrahamu alikuwa anautazamia Mji Ambao Mjenzi na Mwanzilishi alikuwa Mungu. Na leo sisi ni wasafiri, wageni, tukiutafuta Mji Ambao Mjenzi na Mwanzilishi ni Mungu. Tazama! Abrahamu, kabla yeye hajawahi kujulikana, kulikuweko na kitu fulani kama silka ndani yake, kwamba yeye aliutazamia huo Mji.

Leo hii, nikiwa napita chini na mke, nilikuwa ninasema, "Ni mahali padogo pazuri hapa palipokaa juu ya kilima, huenda miaka mia tatu iliyopita, msitu mzuri, mbao kuu ndefu. Mwanadamu aliingia, wakaikatia chini, wakachafua vijito. Pangekuwa mahali pazuri pa kuishi hapa." Naam, lakini angalieni, yeye amejenga nyumba. Ndipo wakaanza kuongezeka. Dhambi na vurugu vikaanza kuingia. Hollywood ikaja karibu na yeye, ikaletwa ndani na sinema, kwa njia ya televisheni. Kwa njia ya … Na sasa pamechafuliwa, pana dhambi, kila jiji!

Na kwa kweli, kama watu, kitu fulani ndani yao kupenda kuishi kwa pamoja, kuwa na jirani, na kuwa mwenye haki. Hakika kuna Mji mahali fulani! Kilindi kikiita Kilindi tena!

28 Na Abrahamu aliuona mji wa siku yake, Uri ya Ukaldayo. Na yeye alijua kwamba kwa sababu kulikuwa na kitu fulani ndani yake kinachoita kwamba kulikuwa na Mji uliokuwa tofauti, Ambao Mjenzi na Mwanzilishi alikuwa Mungu. Na Mungu aliona hilo ndani ya Abrahamu, akamwambia, "Jitenge mwenyewe sasa, toka nje."

Sasa, Abrahamu, jambo moja ninalotaka nione, yeye alitii Neno la Mungu kwa makini.

Siku zote kumbukeni hilo! Huo ndio Ujumbe wangu. Ni lazima ulitii Neno. Na kwa kujua chochote kinyume na Hilo, achana nalo. Inaweza kuonekana vema, lakini usitoe hoja dhidi ya Neno la Mungu.

Hicho ndicho kitu cha kwanza Shetani alichofanya, ilikuwa ni hoja dhidi ya Neno, kwa Hawa. Na kamwe Hawa hakutilia Neno mashaka. Yeye alitoa tu hoja. Shetani alihoji Hilo.

Na hivyo ndivyo wao wanavyofanya leo. "Je, si inaridhisha kwamba tungefanya hili? Je, si inaridhisha?" Kama hilo ni kinyume na Neno la Mungu, achana nalo! Hiyo ni sauti ya Shetani.

29 Hebu Neno, kama Neno liko ndani yako… "Kama mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu ndani yenu, basi ombeni lolote mtakalo." Roho Mtakatifu! "Mkikaa ndani Yangu, Neno Langu ndani yenu," hilo ni Neno lililofanyika mwili, "ombeni lolote mtakalo na litatendeka." Hiyo ndiyo njia. Ondoa kanuni zote za imani ya dini, vitu vyote, na ushikilie Neno kwa sababu hilo ni Kristo. Tazama, ndipo litajidhihirisha Lenyewe.

Mtu fulani alisema, "Ndugu Branham, wewe unajuaje hayo mambo. Kwa vipi?"

Haya mnayoyaona hapa katika mkutano ni mambo ya kujitolea. Mtu yeyote anayesafiri na mikutano hapa, anajua hilo. Roho Mtakatifu hufunua mambo yanayokuja wiki na miezi katikati ya wakati. Na mwulize mtu yeyote,"Je, hilo liliwahi kushindwa wakati wowote?" Haliwezi kushindwa, unaona. "Wewe unajuaje hilo?" Kwa sababu hiyo ni ahadi ya Neno, na ile saa imewadia. Inapasa hilo litukie. Sasa, mimi sijui, kuna wachache sana, wachache watakaoliamini hilo, lakini inapasa hilo liende mbele hata hivyo. Na je, uliwahi kuona, hilo linapita moja kwa moja juu ya kichwa cha watu, na limepita na kutendeka kabla wao hawajatambua hilo. Ni hivyo siku zote.

30 Kwenu watu wa Katoliki, mnajua kile kanisa lenu limefanya? Kwa sababu Joan wa Arc alikuwa mtakatifu halisi wa Mungu, alitenda miujiza ya Mungu, akatabiri juu ya Mungu. Na mkamwita yeye mchawi na mkamchoma moto na kuteketea; na yeye akipiga kelele kwa ajili ya rehema, na mlimchoma kwa moto hadi akateketea. Miaka mamia baadaye, mkatambua mlikuwa mmekosea, ndipo mkamfanya kuwa mtakatifu. Yeye alipita moja kwa moja juu yenu, na ninyi hamkumjua.

Eliya alipita moja kwa moja, wao hawakumjua yeye. "Mzee anayejifanya kuwa

mganga."

Kristo alipita, wao hawakumjua Yeye hadi baada ya kifo Chake, kuzikwa, na kufufuka. Mungu huweka hilo. Na hilo huvuta mivuto kabisa kufunika macho ya asiyeamini. Na ilionyesha…Yeye alisema, "Nalificha hilo machoni pa wenye hekima na akili, na kulifunua kwa watoto kama hawa watakaojifunza." Kristo alimshukuru Mungu kwa kufanya hilo. Unaona?

Jinyenyekeze mwenyewe. Amini hilo. Lijaribu Neno.

Yesu alisema, "Yachunguzeni Maandiko, kwani ndani Yake mnafikiri mna Uzima wa Milele, na hayo yananishuhudia Mimi. Mnapaswa kuwa mmeijua ile saa." Kasema, aliwaambia Mafarisayo, "Enyi wanafiki, mnaweza 11 kutambua uso wa anga. Lakini ishara za wakati, hamwezi kutambua. Kwani kama mngelinijua Mimi, mngeijua na siku Yangu." Lilipita moja kwa moja juu yao, hawakujua hilo hadi hilo lilipokuwa limekwishaondoka. Angalieni sasa Neno likiwa muhimu mno.

31 Na angalieni lingine tunapokuwa kwenye hilo, Lutu. Yesu alisema, Mwenyewe, "Mkumbukeni mke wa Lutu." Kama Neno siyo muhimu mno, kama kutoa hoja ni sawa; wakati yule malaika alipomwambia Lutu na familia yake, "Nendeni Zoari, lakini msitazame nyuma!" Na mke wa Lutu, kwenye kitu kidogo kisicho muhimu kama kugeuka na kutazama nyuma, lakini hilo lilikuwa kinyume na Neno, yeye aligeuka kuwa nguzo ya chumvi.

Ndipo unasema, "Kuwaambia wanawake juu ya kukata nywele zao, kuvaa nguo…? Mungu alisema usifanye hilo! Ufuate Neno. Na Lutu alikuwa, pasipo na shaka, na mke mzuri, lakini yeye hakufuata Amri ya Neno. Lutu! Hawa alikuwa mwanamke mzuri, lakini yeye hakufuata Amri kwenye Neno; yeye alihojiana na hilo kidogo.

32 "Je, hili linaridhisha, Ndugu Branham, kwamba tungefanya hili? Mimi ni raia wa Amerika, mimi-mimi nina haki ya kufanya lolote ninalotaka. Hiyo ni haki yangu ya Kiamerika." Ni haki yako ya Kiamerika, lakini siyo haki ya Kikristo. Kwani, kwa njia ya Kikristo wewe ni kondoo; na kondoo hupoteza haki zake. Yeye hukaa kimya na kukuruhusu uchukue kutoka kwake haki zote alizo nazo. Lakini mbuzi atapigana juu ya hiyo. Hilo ni sahihi. Lakini kondoo hupoteza haki zake. Na Mkristo siku zote hupoteza haki zao za kitaifa kama ni kinyume na haki zako za Kikristo.

Mke wa Lutu akitazama nyuma tu, [Ndugu Branham anadata kidole chake-Mh.] lilikuwa hilo! Sasa hilo lilifanya nini? Hilo linatuambia sisi hapa katika Abrahamu, na Lutu, kuwa kile kitu wao walichoweka kule, ni mfano. Na hatuwezi kuondokana na hicho.

Waebrania, ile sura ya 11, ilisema, "Haya mambo yalikuwa mfano kwetu. Tukiona kwamba tumezungukwa na wingu kuu la mashahidi. Tuweke kando kila dhambi." Dhambi ni nini? Kutokuamini! "Kila dhambi, kila kutokuamini Neno la Mungu, hilo linatusonga kwa urahisi mno."

33 Tunakuja dhidi ya kitu fulani, tunasema, "Vema, wao wanahubiri hilo, kwamba hilo lilikuwa…" Usifanye hilo! Fanya tu kile Mungu alichosema ufanye. Dumu na Hilo, kwa makini!

Unasema, "Hilo halifanyi tofauti yoyote."

Vema, kitu pekee ninachoweza kusema ni kile Neno lilichosema. Na Yesu kwa dhati alisema kwamba, "Mkumbukeni mke wa Lutu." Yeye alitazam tu nyuma juu ya bega lake. Hawa alisita tu kwa kitambo kidogo. Ni hilo tu yeye alilofanya. Mke wa Lutu alitazama tu nyuma. Na kama …Na Mungu alimgeuza yule mwanamume mwenye haki, Lutu, mke wa Lutu kuwa nguzo ya chumvi, kwa kitu kidogo tu, kwa kutokutii tu Amri Yake vya kutosha kwa kutazama tu nyuma na kuona ule moto wote ulikuwa juu ya nini, naye akageuka kuwa nguzo ya chumvi, na imesimama kule hata leo kama mfano kwamba Mungu humaanisha kile Yeye anachosema.

Ee, kama imani halisi ingeweza kutia nanga ndani ya watu! "Imani huja kwa kusikia, kusikia Neno la Mungu."

34 Hawa alisita kwa kitambo kidogo. Ni hilo tu aliloweza kufanya. Shetani alikuwa amempata, na akahojiana pamoja na Hawa. "Je, si haliridhishi? Kama Dada Fulani anaweza kufanya hilo, je, wewe huwezi kufanya, pia? Yeye ni mke wa mchungaji." Mimi sijali yeye ni nani, au ndugu ni nani. Kama hilo ni kinyume na Neno, usilisikilize hilo. Endelea moja kwa moja! Mifano...!

Hivyo ndivyo Abrahamu alivyofanya. Ni kiasi gani cha hoja unachofikiri sayansi ya tiba ingeliweza kumpa yeye, ya siku ile, kuwa yeye hakuwa anakwenda kumpata yule mtoto? Na vipi juu ya wakati yeye alipokuwa na umri wa miaka sabini na tano? Basi tunamwona yeye alipokuwa na umri wa miaka mia, bado yeye aliamini hilo kwa nguvu zaidi kuliko alivyofanya mara ya kwanza, alikuwa na miaka ishirini na tano ya kuendelea kujenga imani zaidi juu ya hilo. Nalipenda hilo. Ndiyo, bwana.

35 Basi nataka kuleta usikivu wenu kwenye jambo fulani lingine kabla hatujasimama. Je, mliona? Na-natumaini kwamba mlilipata hilo. Kwenye lile agano likiwa linathibitishwa, kwa kuandika hilo agano na kulipasua vipande viwili, mlilipata hilo? Inueni mikono yenu juu kama mlilipata, mlipata kile hilo lilichomaanisha. Agano liliandikwa, likapasuliwa vipande viwili, Mungu akichukua udhihirisho wa utatu, akiufanya kuwa mmoja; akipasua vipande viwili, akiupeleka ule mwili Juu, na kumrejesha Roho Mtakatifu ili aishi ndani ya Kanisa, ili kuzaa kitu kile kile ambacho huo mwili ulizaa, kama mke, Bibiarusi; Roho yule yule, matendo yale yale, Fundisho lile lile, kila kitu sawasawa tu jinsi Yeye alivyokuwa nacho, ishara ile ile, "Yesu Kristo yule jana, leo, na hata milele na milele." Tazama!

Panaweza pakaweko na, labda, Myahudi aliyeketi hapa.

Unaona, Mungu hufanya hayo mambo, na linakwenda moja kwa moja miongoni mwa watu na bado wao hawalipati hilo.

Kama ambavyo nilikuwa nikielezea juu ya kwa nini wanawake hufunika uso wao wanapoolewa. Kwa nini? Huenda wao wasielewe hilo. Lakini kile wao wanachofanya, ni, wakijua wao ni mwili, wao hawana kichwa, mwanamume ndiye kichwa chao. Hiyo ndiyo sababu Rebeka alijifunika mwenyewe. Na hiyo ndiyo sababu Kanisa linapaswa kujifunika lenyewe na kujisalimisha lenyewe kwa Kristo, kwa sababu Yeye ndiye Kichwa, na Yeye ndiye Neno.

36 Sasa, Myahudi, ile Yomu Kippur, wanapokula ushirika, au Pasaka, kila mmoja anajua, ambaye ni Myahudi, na anajua kuwa chini ya kifuniko kuna kipande cha mkate kilichovunjwa. Na hakuna Myahudi ninayemjua, niliyewahi kuzungumza naye, anaweza kueleza ni kwa nini hicho kipande cha mkate kilivunjwa. Kwa nini, liko hapa katika uthibitisho wa lile agano, mwili wa Kristo uliovunjwa, Yeye alipomvunja Mungu kutoka kwa mwanadamu; Yeye alikuwa yote mawili Mungu na mwanadamu. Na Yeye alipomchukua Roho … Na Yesu alisema, sikilizeni, "Penye ile siku mtajua kuwa Mimi ni ndani ya Baba, Baba ndani Yangu; Mimi ndani yenu, na ninyi ndani Yangu." Ni Mungu ndani ya watu Wake! Mungu yule yule!

Yeye aliwakilishwa pale, pale tulipozungumza jioni iliyopita. Mungu alishuka chini, kwa herufi kubwa B-w-a-n-a, Yehova-Yire, Yehova-rafa, Yehova-manase, Elohim, Yeye anayejitosheleza, Mwenye Nguvu, Mwenye Matiti, vyeo Vyake vyote na kila kitu, vilidhihirishwa katika mwili wa mwanadamu uliokula chakula cha kibinadamu, na kutoweka mbele zao. Mungu!

37 Na Yesu, Yeye alipokuja, Yeye alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku ile, ndivyo itakavyokuwa." Mungu!

Huo ni mkate uliovunjwa chini ya kifuniko, kipande kilichovunjwa; siyo kile wao wanachochukua, bali Kile kilichovunjwa. Kwa nini wao hawaelewi hilo?

Kitu kile kile Yesu alipochukua vile-vile vipande vya ngozi na kuanza kusoma. Yeye alisoma sehemu ya aya, na kuiacha, ile sehemu yake iliyobaki, kwa sababu ilikuwa tu kwa ajili Yake kwa ajili ya siku ile. Ile sehemu nyingine ya ile aya ilihusika na Kuja Kwake kwa Pili.

Hiyo ndiyo sababu Wayahudi hawaelewi kuwa, kwa sababu iliwapasa wapofushwe. Wao hawakumwona Masihi wao, na bado Yeye alikuwa pale. Na kila wakati walipochukua Pasaka yao, kunakuwa na mkate uliovunjwa tena, na pasipokujua hilo.

Nilimwuliza rabi. Yeye alisema, "Sisi tumefundishwa kufanya hilo."

Nikasema, "Kwa nini mnafanya hilo?"

Yeye akasema, "Mimi sijui. Hakuna mtu mwingine anayejua."

Ona, mwanamke hufunika uso wake, na bado yeye hatambui. Badala ya kuingia ndani na kumwacha mume wake awe kichwa chake, yeye anakuwa kichwa cha mume. Huo ni upotofu. Sasa huo ni mtazamo wa Kiamerika.

Lakini ndilo hilo, mkate uliovunjwa. Ndipo tunaona tena. Nataka muandike, ninyi, katika kuweka msingi sasa kabla hatujafikia ile sehemu halisi tunayotaka kunena juu yake jioni hii.

38 Usiku uliopita mnakumbuka kuwa wakati Abrahamu, lile agano lilifanyika kwa Abrahamu na Uzao wake baada yake. Sasa, kulikuweko na uzao wa asili wa Abrahamu, kwa njia ya tendo la imani lilizaa huo; lakini ule Uzao halisi wa Abrahamu ulikuwa Kristo, Biblia…ambao ulikuwa Uzao wa kifalme wa Abrahamu. Sasa, tazama.

Abrahamu, kabla ya maangamizi ya moto katika siku yake, kulikuweko na ishara iliyofanyika kwa Abrahamu. Kundi lake teule. Na hiyo ilikuwa, Mungu alishuka chini katika umbo la mwanadamu, akigeuzia hema kisogo toka pale Sara alikokuwa, na kusema kile Sara alichokuwa akisema ndani ya hema. Na Yesu alikuja pale na alisema jambo lile lile lingekuweko penye mwisho wa kipindi. Sasa, huyo alikuwa Abrahamu.

Ndipo uzao wake wa asili, Masihi atakapokuja. Na Simoni alimjia Yesu, na Yeye akamwambia jina lake lilikuwa Simoni, na alikuwa mwana wa Yona, alijua siri za moyo wake. Alimwambia Filipo…au Natanaeli, kuwa Filipo alikuwa, "Nilikuona wewe ulipokuwa chini ya mti." Alimwambia yule mwanamke pale kisimani, "Unao waume watano." Na yeye akasema, "Bwana natambua Wewe ni nabii." Unaona, mwisho wa uzao wa kimwili wa Abrahamu ulipata hiyo ishara.

Na hilo lilibashiriwa na Mzao wa kifalme Mwenyewe, Kristo, kuwa ule Uzao wa kifalme, mwishoni mwa siku zao, ungelikuwa na kitu kile kile. Sasa ninatumaini tunalipata hili.

39 Alimbadilisha…. Angalia, Mungu alibadilisha jina la Abrahamu. Ni bora niondoke kwenye hilo. Nitakaporudi kwa ajili ya uamsho mrefu, tutaingia katika hilo. Ilipasa yeye abadili jina lake kutoka kwenye jina lake la kidunia, kwenda kwenye jina alilopewa na Mungu.

Unasema, "Jina la mtu ni nini kwetu, chochote?" Loo, ndugu, kama tu ungejua! Mbona, baadhi ya haya majina ya kisasa tuliyo nayo! Sitaki kuyataja hayo, kwa sababu hilo litaumiza hisia zenu. Lakini Mungu anayo majina yanayomaanisha mambo, hilo hubadilisha mwenendo mzima. Ee, unasema, "Upuuzi!"

Vipi juu ya-vipi juu ya Yakobo? Kabla yeye hajafanyika mwana wa mfalme mbele za Mungu, ilimbidi yeye abadilishwe jina lake kutoka Yakobo kuwa Israeli. Je, hilo ni sahihi? Hakika. Paulo; Sauli alimpasa jina lake libadilishwe kuwa Paulo. Ee, ni wangapi tungeweza kuwataja, na kusema kuwa Mungu alibadilisha jina lao! Abramu kuwa Abrahamu, Sarai kuwa Sara, akibadilisha jina lao. Loo, jamani! Ni baraka iliyoje, kuingia katika kanisa fulani dogo likiwa na kundi teule, na kwenda kufundisha hilo, unaona haleluya katika moyo wao, unapoona kile Mungu anachofanya.

40 Sasa, jioni iliyopita nilikuwa nikieleza juu ya "katikati ya msitari" na "kuthibitisha hilo." Nataka tu kuligonga hilo tena kabla sijaingia katika somo. Kwamba, Mungu alimbadilisha Abrahamu kutoka mwanamume mzee mwenye makunyanzi, yeye na Sara, kurejea kwenye watu wawili walio vijana, alibadilisha hali yao ya kimwili kabla wao hawajaweza kumpokea yule mwana wa ahadi. Ishara ya mwisho waliyopata ilikuwa udhihirisho wa Mungu katika mwili, aliweza kusoma moyo wa mwanamke nyuma Yake, katika hema. Na jambo lililofuata lilikuwa kwamba miili yao ilibadilishwa. Sasa, jioni iliyopita nilikuwa ninachelewa, na niliweza kuhisi baadhi wakishangaa kuhusu hilo. Nataka bado nililete hilo karibu zaidi kidogo.

Sasa, uthibitisho wa hilo ulikuwa kwamba, wakati wote wawili walipokwenda ile safari ndefu, walikuwa wamebadilishwa kabisa. Na Biblia ilisema, "Wote wawili wamechukuliwa na umri. Na mwili wa Abrahamu ulikuwa kama uliokufa, na tumbo la uzazi la Sara lilikuwa limekufa." Je, hilo lilikuwa sahihi? Tunajua wao walikuwa wamekufa, lakini Mungu aliwabadilisha. Sasa ili kuwathibitishia hilo, kwamba Yeye alifanya hilo. Kwanza, kwa nini yule Mfilisti (au siyo niniii…) ndiyo, naamini alikuwa mfalme wa Wafilisti, alimpenda Sara, mwanamke mzee? Na Sara alikuwa mzuri wa sura.

41 Jambo lingine. Isaka alipozaliwa, na Sara na Abrahamu walikuwa na umri mkubwa, wakiwa tayari kufa, ndipo wakaishi, na Isaka akaoa alipokuwa na umri wa miaka arobaini; Sara akafa. Na Abrahamu akaoa mwanamke, Ketura, na alikuwa nao watano, sita wana, naamini ilikuwa hivyo, mbali na mabinti, baada ya hilo; na hapa, miaka sitini iliyopita, yeye alikuwa kama aliyekufa! Ke-t-u-r-a, Ketura. Yeye alimwoa Ketura, miaka

hamsini au sitini baada ya hilo, naye alikuwa na wanawe sita mbali na mabinti zake; na miaka sitini hapo kabla, yeye alikuwa kama aliyekufa. Haleluya! Hilo ndilo jambo lenyewe! Ahadi ya Mungu ni hakika. Amina. Loo, nalipenda Hilo!

Ulipate tu wewe mwenyewe na kusoma… Leo hii, kule nyuma msituni, nikiwa ninasoma, nilipata kitu fulani kidogo ninachotaka kueleza.

42 Israeli. Hao watu wa Mungu siku moja walikuwa kule chini Misri, waliuzwa utumwani, nao wasingeweza kujizuia kuwa kule. Mpango mkuu wa Mungu uliojulikana tangu asili uliwapeleka kule. Yeye alikuwa amemwambia Abrahamu wao wangelikaa katika nchi ya ugenini kwa miaka mia nne. Na huko wakawa kama hao watu wengine, nao walikuwa watumwa. Kama-kama mwanamume wa Kimisri alitaka kuwachukua wasichana vijana wa Kiebrania kwa nguvu, hakuna ambacho kingeweza kusemwa. Kama wao walitaka kuua vijana wanaume, waliwaua, hakuna ambacho kingesemwa. Wao walikuwa watumwa. Waliwatolea nje mikate ya kusukumwa. Wakaila hiyo, au kutokuwa nayo; wakilalamika, wanauawa! Ni mahali pa jinsi gani kwa ajili ya watu wa Mungu.

43 Lakini siku moja, haleluya, Mungu alikumbuka ahadi Yake kwa Abrahamu. Utukufu! Sasa naanza kujisikia wa kidini tena. Tazama, Mungu aliikumbuka ahadi Yake kwa Abrahamu. Na Yeye alimpaka mafuta nabii, kwa Nguzo ya Moto juu yake, naye akaja chini katika ile nchi na kuanza kuwakumbusha juu ya ahadi ya Mungu ambayo isingeweza kushindwa. Na Mungu alikuwepo ili kuthibitisha Neno Lake. Sawa. Yeye aliwaambia juu ya nchi iliyokuwa ikitiririka maziwa na asali, Mungu alikuwa amewapa wao hiyo. Wao walitembea kutoka Misri juu ya nguvu za ushuhuda wa huyu nabii pamoja na Nguzo ya Moto juu yao, kwa sababu yeye alitumwa. Na Mungu alikuwa amethibitisha kuwa Yeye alikuwa pamoja nao.

44 Sasa walipofika mahali panapoitwa Kadeshi-barnea. Hapo palikuwa kiti cha hukumu cha ulimwengu wakati mmoja, Kadeshi-barnea. Na kule walikuwa na shujaa miongoni mwao, kwa jina la Yoshua. Na neno Yoshua, katika Kiebrania, humaanisha "Yehova-mwokozi." Na Yoshua, shujaa mkuu…Sasa kumbukeni, wao hawakuwa wamewahi kuiona hii nchi, walikuwa wamesikia tu juu yake. Mnaona huo mfano sasa? Walikuwa wamesikia tu juu ya hiyo nchi. Wao walikuwa wameacha vyote ili kwenda kwenye hii nchi, kwa sababu Neno la Bwana lilikuwa limeletwa kwao na kuthibitishwa kuwa wao walikuwa njiani mwao kwenda kwenye hii nchi. Ni mfano wa Kanisa ulioje, njiani mwao, pasipo kujua chochote juu yake, hakuna mmoja wao aliyewahi kuwa kule. Lakini Yoshua, walipokaribia mpakani, pale Kadeshi, kiti cha hukumu, pale hukumu ilipowapiga Israeli, kutoka kwa yeye aliyekuwa amefika kule na kurejea. Na Yoshua alivuka Yordani, kule kuingia ile nchi ya ahadi, na kuleta ushahidi kwamba ilikuwa kabisa tu kile Mungu alichosema ilikuwa. Nao waliweza kuonja zabibu zilizolimwa katika ile nchi ya raha kikamilifu.

45 Sasa, wao walikuwa wameahidiwa kuwa wangeweza kuwa nyumbani ambapo wangeweza kuwa huru, wangeweza kulea watoto wao katika uadilifu na-na kumcha Mungu, wawe na kanisa, na kadhalika. Wao walikuwa na furaha iliyoje kuvuka kwenye ile nchi na kufika nyumbani, kutoka kuwa watumwa. Tazama. Lakini wao walipovuka, kule waliishi maisha yao, lilikuwa jambo kuu. Lakini hatimaye zile pande za milima ikakandikwa kwa mawe ya makaburi. Walizeeka na kufa, walizeeka na kufa. Watu wa Mungu.

Ndipo siku moja kukaja Shujaa mkuu mwingine, mkuu zaidi ya hao wote, Yehova-Mwokozi, Yesu, Yeye alikuja, na Yeye akasema, "Kuna Uzima ng'ambo ya mauti! Kwani, katika Jumba la Baba Yangu kuna majumba mengi. Kama haikuwa hivyo ningeliwaambia. Nitakwenda na kuwaandalia mahali, na kurudi tena kuwapokea Kwangu Mwenyewe." Na huyu Shujaa mkuu alikuja kwa Kadeshi-barnea Yake, kile kiti cha hukumu kwa ajili yetu sisi sote, Kalvari! Pale Yeye alichukua ju Yake maovu yetu yote. Na Yeye alivuka mto Yordani tunaouita mauti. Na penye siku ya tatu Yeye alifufuka tena, kama Yoshua akiwa anarejea kuvuka mto, akileta ushahidi kuwa yule mtu aliyekufa anaweza kuwa hai tena."

46 Na Yeye alisema, "Ili kuwafanyia uhakikisho, nataka mwende juu kule kwenye mji wa Yerusalemu, na msubiri huko. Nitawapa amana Yake. Nitawapa ushahidi, malipo ya awali." Nao walikwenda hadi mjini Yerusalemu na wakasubiri hadi Uzima wa Milele ulipokuja kama upepo wenye nguvu unaovuma.

Na leo, baada ya miaka elfu mbili, bado tunao huo ushahidi kuwa tumepita kutoka

mautini kuingia Uzimani. Yoshua wetu amerejesha ushuhuda, na tuko njiani mwetu kwenda Nchi ya ahadi, tukionja karama za Mungu za kimbinguni ambazo Yeye amezirejesha kwetu. Tazama hilo, ni la ajabu iliyoje! Tazama pale wewe ulipokuwa wakati mmoja. Mlevi…

47 Nilikutana na ndugu fulani leo; yeye alikuwa na kujisikia kusiko kwa kawaida na kugeukia barabara fulani na kwenda zake. Nasahau jina la huyo mtu lilikuwa nini. Huenda yeye yupo hapa katika mkutano. Na bado, kama yeye hayupo, mbona, Mungu alikuwa mwema kwake. Yeye ni Mhindi, Mhindi kwa sehemu. Yeye anatokea Virginia. Roho Mtakatifu aliniambia, siyo kusema hilo. Nilikuwa nimemwachia mke wangu atoke. Akasema, "Uende chini njia hii, na upinde kona hii." Nilikwenda chini kule. Ee, hilo hutokea wakati wote. "Subiri hapa hapa." Ndipo nilingoja pale kwa dakika chache. Akasema, "Geuka na urudi kuelekea njia hii." Na nilipofanya hivyo, nilikutana na yeye.

Yeye akasema, "Ndugu Branham, nakufahamu." Kasema, "Nilikuja Jeffersonville wakati mmoja, na kukuona." Na kusema mimi … "Wewe ulikuwa nchi za ng'ambo." Lakini yeye alikuwa mlevi, katika maisha yake. Nikaushika mkono wake, pasipo yeye kujua kile nilichokuwa nikifanya. Naye alikuwa na ugonjwa wa kuua seli za ini. Nilipokuwa nimesimama pale nikiwa nimeshikilia mkono wake, ule mtetemo uliniacha. Nini? Yeye aliponywa. Pale pale kwenye kona ya barabara, wao wamesikia hilo katika jiji lenu.

48 Simjui mtu yule…Je, yeye yupo hapa? Sijui. Kama yupo, yeye…Mimi sijui. Yeye alisema alikuwa anataka kurejea nyumbani. Naamini ilinipasa kwenda. Yeye alikuwa mwanamume wa Kihindi, nafikiri alikuwa ameoa mwanamke mzungu. Na yeye alikuwa anatokea Virginia. Na nilisahau jina lake lilikuwa nini. Yeye aliishi chini hapa Lagor au kitu kama hicho. Na amekwenda kote hadi Jeffersonville. Lakini yeye na kujisikia kutembea kwenye ile kona; Roho Mtakatifu alisema, "Uende chini njia hii." Ewe Mungu, uturehemu! Hilo ndilo jambo lenyewe.

Ningeweza kuchukua masaa baada ya masaa, ya kuwaambia ninyi mambo yale niliyoyaona yakitukia na kufanyika namna hiyo. Kwa nini? Yesu, Shujaa wetu mkuu, alikwenda kule na kuiteka ile nchi, akayashinda mauti, akaishinda kuzimu, akalishinda kaburi, akafufuka siku ya tatu, na kusema, "Mimi Ndiye niliyekuwa nimekufa, na niko hai tena milele na milele, nami ninazo funguo za mauti na kuzimu." Huyo hapo Mshindi, kwani Yeye alilichana pazia vipande viwili. Yeye amesimama hapo!

49 Kama dada mweusi wa kale. Samahani, marafiki zangu weusi ndani hapa. Yeye alikuwa anatoa ushuhuda katika mkutano, naye alikuwa wa kusini mno katika kuongea kwake. Alisema, "Vema, nataka niwaambie ninyi nyote jambo fulani jioni hii." Akasema, "Hakika mimi sicho ninachopaswa kuwa." Na yeye akasema, "Nina hakika mimi sicho ninachotaka kuwa. Lakini, jambo moja najua, mimi sicho nilichokuwa." Hivyo yeye alikuwa amefika mahali fulani.

Na nasema, ndilo hilo jioni hii! Wakati mmoja tulikuwa tumepotea katika dhambi. Na leo, kwa kukubali ushahidi, ile ahadi iliyorudishwa (malipo ya awali juu ya wokovu wetu wa Milele) tumefufuka kutoka mautini kuingia Uzimani, na tunaishi juu ya hilo. Itakuwaje tutakapofikia malipo kamili, na kuvuka kule mtoni, sisi wenyewe, katika ile Nchi ya utukufu?

50 Jaribu kuu… Sasa Abrahamu baada ya haya mambo yote mazuri, yeye alijaribiwa baada ya yeye kupokea baraka. Abrahamu alijaribiwa.

Sasa hapo ndipo watu hushindwa. Sasa, sikiliza kwa makini hasa sasa, usilikose hili. Biblia ilisema, "Kila mwana ajaye kwa Mungu lazima arudiwe, aadhibiwe, achapwe kiboko. Na kama hatuwezi kustahimili adhabu, tunafanyika watoto haramu, na siyo watoto wa Mungu." Hilo linathibitisha kuwa imani yetu haikuwa ile tuliyoisema, hatuna kile tulichokiri kuwa nacho. Sasa tunafikia chini katika Ukalvini mzuri hasa sasa, hivyo inatupasa kutazama hilo. Sasa angalia, "Kila mwana ajaye kwa Mungu lazima arudiwe, aadhibiwe," Neno humchapa kiboko yeye na kumkata vipande vipande, linagongolea mbali kila kanuni ya imani ya dini kutoka chini yake; unaona, anajaribiwa, na kuona kama yeye ni mwana wa Mungu.

Sasa Abrahamu, baada ya yeye kupokea baraka, ndipo alipojaribiwa baadaye.

51 Ule wakati umekwenda wapi? Hata sijamaliza somo langu, na ni wakati wa kufunga. Je, mtanivumilia dakika nyingine kumi na tano? [Kusanyiko linasema, "Amina."-Mh.]

Asanteni. Iweni wanyenyekevu. (Abrahamu. Mtazame Nuhu.) Hebu tulichukue hilo kwa kitambo kidogo. Hatuwezi kuharakisha; hakuna haja. Na, jamani, tunaharakishia nini? Nakwenda pole pole tu. Mimi-mimi siko kama baadhi ya hawa jamaa ambao wanaweza kusimama, wanaoweza tu kulipepea hilo liondoke namna hiyo. Mimi-mimi mimi nakwenda pole pole, inanipasa nisubiri hadi Yeye anipe mimi hilo.

Mtazame Nuhu, baada ya Mungu kumfanya yeye ahubiri miaka mia na ishirini, pale pale katikati ya ulimwengu wa kisayansi mkuu zaidi kuliko tulio nao leo. Ee, hakika, wao walijenga mapiramidi. Tusingeweza kujenga hizo. Walijenga Sanamu kubwa lenye sura ya mwanadamu. Tusingeweza kujenga. Wao walipaka miili dawa ili iweze kuonekana ya kiasili. Hatuwezi kufanya hilo. Wao walikuwa na rangi ambayo waliweza kuweka katika vitu, ambapo hiyo rangi isingeweza kamwe kubadilika kwa miaka elfu nne. Sisi hatuna hiyo. [Sehemu tupu kwenye kanda-Mh.] Na hilo linaonyesha wao walikuwa na ustaarabu kama ule Yesu aliosema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu." Na Nuhu, katika ule ulimwengu wa kisayansi, akihubiri, "Mvua inakwenda kunyesha kutoka mbinguni, kwa sababu Neno la Mungu lilisema hivyo! Nuhu alikuwa nabii.

52 Na mnapowaona manabii wakiinuka, ni bora mkatazama, hukumu iko njiani mwake.

Hivyo basi Nuhu akiwa anahubiri, na watu wakilikataa hilo, walicheka mbele zake. Naweza kuwazia baadhi yao wakisema, "Hilo halikubaliani na uthibitisho wetu wa kisayansi." Loo!

Nawazia, ni kitu kile kile kama ilivyo leo. Wanasema kwamba, "Kupiga kelele na kumtukuza Mungu, na kulia, na huyu hapa anayeitwa mtakatifu anayejiviringisha maisha na vitu, hayo yote ni kazi za msisimko." Hilo halikubaliani na uthibitisho wao wa kisayansi, bali linakubaliana na Biblia ya Mungu. Hilo ndilo jambo la msingi. Angalia.

Nawazia sayansi ikitoka nje na kusema, "Tazameni, jamaa. Tazameni, ninyi-ninyi ni kama mliorukwa na akili. Tazameni hapa. Mimi, tunayo rada, tunaweza kuupiga picha mwezi au kutuma chombo cha uchunguzi kwenda angani juu kule. Hakuna hata tone moja la maji kati ya hapa na huko. Sasa hiyo inatokea wapi?"

Naweza kumsikia Nuhu akisema, "Mungu alisema hivyo! Na kama Mungu alisema ilikuwa hivyo, Yeye ni Yehova-Yire, Yeye anaweza kujipatia maji juu kule. Mungu alisema hivyo! Linakwenda kutukia, kwa vyovyote vile! Mtu fulani alisema…

53 Mchukue mtu anayekufa kwa saratani, ni kivuli cha mtu, yeye yupo hapa; mwaka unaofuata yeye ni mtu mwenye afya nzuri. Hilo linatokeaje? Ilimlaza yeye…Ninazo mamia ya hizo shuhuda. Mtu ambaye alikwishaondoka kwenye haya maisha, na daktari aliweka sahihi tamko, "Yeye amekufa, amekwishakufa kwa saa kadha." Na Mungu akatoa ono, na yeye anaishi sasa. Kwa vipi? Msiniulize mimi. Sijui. Lakini Mungu alisema, "Ponyeni wagonjwa, fufueni wafu, toeni mapepo." Hilo ni sahihi.

Unapokuwa mgonjwa na Mungu anakutangazia uponyaji, uende tu kwa daktari wako, hebu yeye akuambie ulipokuwa mzima. Yeye atakupa…Hilo litatoa ushuhuda kwake. Yeye anaposema, "Vema, hilo limekwisha ondoka;" unasema, "Mungu asifiwe! Asante, daktari, kwa huduma zako." Unaweza kwenda nyumbani. Unaona? Hilo ni sahihi.

54 Tazama.

Sasa Nuhu, yeye alisema, "Mvua itanyesha, ulimwenguni mwote, inakwenda kuwafutilia mbali ninyi watu waovu."

"Lo, upuuzi! Tunayo makanisa yetu. Mchungaji wetu hasemi kitu chochote kama hicho. Yule mzee amerukwa na akili, akiwa anajenga safina juu kule. Je, unafikiri mtu yeyote ataliamini hilo?"

Siku moja, Mungu alisema, "Nimesikia dhihaka zao vya kutosha. Niko tayari sasa. Ingia ndani!" Na hapa wanyama wakaja, wawili wawili, kasuku dume na jike, korobindo dume na jike, mbuzi dume na jike, kondoo dume na jike, simba, chui, wote hao wanaopumua pumzi juu ya nchi, waliingia ndani ya safina.

Nuhu alisema, "Hiyo ni ishara yenu ya mwisho."

Nao wasingeliamini hilo. "Endelea na uishi pamoja na wanyama wako wanaonuka."

Yeye alikuwa pale, Nuhu akimtii Mungu. Haidhuru ulimwengu ulisema nini, yeye alimsikiliza Mungu; yeye alikuwa nabii. Yeye aliingia ndani ya safina, na Mungu akafunga

mlango nyuma yake.

55 Sasa naweza kuwazia, baadhi ya waamini wa mpakani, walioketi pale na kusikiliza ujumbe wa Nuhu, na kwenda kando, unajua, wao walisema, "Unajua nini, yule mzee huenda alikuwa sahihi. Hebu twendeni kule juu na tusimame pale. Yeye alisema, 'Inakwenda kuanza kunyesha ule mlango utakapofunga.' Mungu alimwambia Yeye angelifunga huo mlango, ilikuwa inakwenda kunyesha, tutabisha hodi mlangoni. Kwa vile yeye ni mzee mwenye moyo wa huruma, atafungua mlango."

Unaona, wakati fulani mnatazama mjumbe badala ya Ujumbe. Mungu aliufunga mlango. Haidhuru Nuhu alikuwa na moyo wa huruma iliyoje, ilikuwa ni Mungu aliyefunga na kufungua, chochote Yeye anachotaka.

56 "Ndugu Branham, kuna mtu aliyeketi chini hapa penye kona. Uende ukamponye, tutaamini katika uponyaji wa Kiungu." Huyo ni yule Mwovu.

Huyo huyo alisema, wao walipomzungushia tambara usoni Mwake na kumpiga juu ya kichwa, na katika uani yeye alisema, "Kama Wewe ni nabii, tuambie ni nani aliyekupiga Wewe sasa. Tutaamini hilo." Yeye hafanyi mzaha kwa yeyote. "Kama Wewe ni Mwana wa Mungu, geuza haya mawe kuwa mkate. Kama Wewe ni Mwana wa Mungu." Yeye angeliweza kufanya hilo, lakini Yeye hafanyi mzaha kwa yeyote. "Kama Wewe ni Mwana wa Mungu, shuka msalabani." Yule kiongozi wa dini alikuwa anasema hilo, unaona. Yeye hafanyi mzaha kwa yeyote.

Yeye alifanya tu kama Baba alivyomwonyesha Yeye, na siyo kingine chochote. Hilo ndilo Yeye alilosema, Mtakatifu Yohana 5:19, "Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe, ila lile ambalo amwona Baba analitenda." Hilo ndilo jambo lenyewe.

57 Tazama.

"Tutakwenda kule na tusimame pale penye safina, kama ikianza kunyesha…"

Namuwazia Nuhu akisema…Yeye aliingia katika orofa ya kwanza, akakwea hadi orofa iliyofuata (hao ndege) kutoka kwenye vitu vitambaavyo hadi kwenye ofisi iliyofuata. Kutoka kuhesabiwa haki, hadi kwenye utakaso (ndege), ndipo yeye alipokwenda kutoka kwenye hilo kuingia katika Ubatizo wa Roho Mtakatifu; pale dirisha lilipokuwa, pale ambapo mwanga ungeweza kuingilia ndani. "Nilifika mbinguni, nikaketi chini." Kasema, "Vema, familia, ninyi mnaokuja ndani hapa pamoja na mimi, asubuhi…Tunachelewa alasiri hii sasa. Sasa Mungu aliufunga ule mlango chini pale. Asubuhi, kutakuweko na giza duniani kote. Asubuhi, mvua zitanyesha na safina itaelea, na Mungu ataatampunguza kila mmoja wa hao wenye dhambi walio wakatili ambao hawakuamini huo Ujumbe." Wote wakiwa wanasubiri.

58 Asubuhi iliyofuata, akaamka, akatazama nje, ni kuzuri na kunakong'aa. Yeye akaingia katika safina, ni wangapi wanaojua ni siku ipi yeye aliyoingia ndani? Siku ya 17 Mei, Nuhu alipokuwa na umri wa miaka mia sita. Siku ya 17 ya Mei, Biblia ilisema hivyo. Na alipoingia ndani, siku ya 17 ikapita, jua likachomoza lenye joto tu kama ambavyo limewahi kuwa.

Ningewazia hao, wa mpakani, wakisema, "Loo! Niliwaambia ninyi hapakuwepo na kitu chochote kwenye hilo! Ninyi nyote mmekaa hapo kwa ajili ya nini? Ondokeni kwa huyo tapeli!"

"Vema, nadhani hilo lilikuwa sahihi."

Lakini, unaona, kuna msitari wa utenganisho uliochorwa kati ya kuamini na kutokuamini. Na ama wewe uje upande mmoja au ule mwingine. Na kuna wakati unapopokea wito wako wa mwisho.

Hivyo, siku ya pili, ni kuvunjika moyo iliyoje kwa Nuhu na kanisa lake, yeye alipowaambia Mungu anakwenda kuangamiza ulimwengu. Lakini unajua ni muda gani alikaa nje? Siku saba, hakuna chochote kilichotokea. Jaribu!

59 Ndipo penye siku ya nane, kulikuweko na giza duniani kote, matone makuu makubwa yakaanza kuanguka kutoka angani, maji yakaanza kumwagika, na chemchemi zakaanza kupasuka. Barabara zikajaa maji. Watu wakabisha hodi mlangoni, lakini Nuhu hakuweza hata kuwasikia. Na hiyo ikaelea juu ya kilima kirefu zaidi ya vyote, na wote waliokuwa nje ya safina waliangamia.

Mungu akimpa Nuhu jaribu, ili kuona kama yeye angejaribu kukwea nje kwenye

dirisha, au kitu fulani. Baada ya kuwa Yeye ameiweka ile ahadi, Nuhu alikaa tuli!

Hilo ndilo jambo lenyewe! Unapokuwa na ahadi, nawe unajua hiyo ni ahadi, dumu nayo! Ilimpasa Abrahamu ajaribiwe. Dumu na ahadi!

Sasa, wao walikuwa na ishara yao ya mwisho. Ndipo mwili wao ukabadilishwa. Na kwa haraka Isaka mdogo alitokea penye sehemu ya tukio, mvulana mzuri mdogo wa Kiyahudi, ningewazia baada ya siku zake nane yeye alitahiriwa. Vipi yule mama kijana, mwenye umri wa miaka mia…Vipi yule Abrahamu, akiwa na umri wa miaka mia; au Sara akiwa na tisini na Abrahamu akiwa na miaka mia; wao wangeweza kuwaje, mnamo miaka ishirini, wakishangilia. Huyu jamaa mdogo, yeye alikuwa mzuri iliyoje…

60 Na unajua, Mungu alisema, "Sasa katika kuwafanya watu katika siku zijazo (ule Uzao wa Abrahamu) wajue, Uzao wako ujue kuwa Mimi naishikilia ahadi Yangu kwa mtu wangu ambaye atalishikilia Neno Langu, nitampa yeye jaribu."

Wakati yule mvulana mdogo alipofikia umri wa miaka kumi na nne, nawazia, nywele ndogo zilizokuwa timtim bila mpango mzuri, na macho madogo mazuri. Ee, ni furaha iliyoje kwa hao baba na mama! Mnajua jinsi ninyi wazazi mlivyo na mtoto wenu, mtoto pekee. Ndipo Mungu akamwambia Abrahamu…Sasa, Yeye asingelimwambia Sara hilo, kwa sababu Sara alikuwa chombo kidhaifu zaidi. Na hivyo Yeye alisema, "Abrahamu, nataka umchukue huyu mvulana mdogo niliyekupa, yule ambaye nitakufanya wewe baba wa mataifa kwa yeye, na nataka umpeleke juu ya mlima nitakaokuonyesha jioni hii, katika ono, na ndipo umwue yeye." Kuangamia kwa tumaini pekee lililokuwepo kwake kuwa baba wa mataifa, ili Mungu atimize Neno Lake; Mungu alisema, "Nitakufanya kuwa baba wa mataifa." Sasa Abrahamu alikuwa amesubiri miaka yote hii, hadi akawa na umri wa miaka mia, umri wa miaka mia na kumi na nne. "Na hapa kuna huyu mvulana mdogo sasa, na ushahidi pekee ulio nao kwamba Mimi nitashikilia Neno Langu, uende kule juu na ukauangamize huo. Bado Mimi nitakufanya baba wa mataifa kwa njia ya huyu mtoto."

61 "Na Abrahamu," kasema, "yeye hakuyumba penye ile ahadi ya Mungu. Yeye alijua kuwa yeye alimpokea mtoto kama mmoja aliyetoka kwa wafu. Alijua, kama Mungu aliahidi hivyo, Yeye angeweza kumfufua kutoka kwa wafu."

Na ndipo sisi ni Uzao wa Abrahamu? Na kosa moja dogo la kitholojia linaweza kulipukia njiani, ili kuwa maarufu kwa hao wanaume na wanawake wengine, mnaliendea hilo badala ya kudumu na Neno. Mwone aibu! Shirika fulani kubwa la dini, hilo linamaanisha nini kwa Mungu? Yeye atalifagilia mbali hilo namna hiyo! [Ndugu Branham anadata kidole chake-Mh.] Yeye yuko mbali na hilo, amekuwa hivyo tangu walipounda shirika la dini, kila moja ya hayo, na siku zote atakuwa hivyo. Siyo watu binafsi ndani mle, bali ule mfumo wa shirika la kidini, uko kinyume na Mungu. Kila kanisa lililojiunda kuwa shirika la dini ni mama…au binti wa shirika la dini la Katoliki. Biblia ilisema hivyo, Ufunuo 17, "Yule kahaba mkuu wa kale, na mabinti zake makahaba." Sahihi kabisa.

62 Tunaye akiwa ameketi hapa hapa sasa juu ya taifa letu. Aibu kwenu Wa-Democrat wazuri mliouza haki yenu ya kuzaliwa! Vema, tutaliacha tu hilo liende, hili, hadi nitakaporudi. Tazama. Nachelewa. Je, Kristo wenu hamaanishi zaidi kwenu kuliko siasa zenu? Mnapaswa kufanya kile Abrahamu Lincoln alichosema wakati ule. Vema. Tazama, tunasonga mbele.

Sasa Mungu alisema, "Mchukue yule jamaa mdogo, mpeleke juu kule penye kilele cha mlima."

Sasa mnataka kujua kama Abrahamu alikuwa mwanamume kijana au la? Yeye alikwenda safari ya siku tatu pamoja na mtoto, akiwa na kuni, pamoja na mtumishi, na punda. Sasa mwanamume yeyote, mwanamume wa kawaida…Mimi nilikuwa zamani nikifanya doria njia za umeme, nilikuwa zamani nikitembea nikiwa mkuu wa hifadhi ya wanyama pori; na niliweza kutembea, kwa urahisi, maili thelathini kwa siku. Na tulikuwa na miguu ya mafuta ya gari, tunaliita hilo. Lakini wale watu, usafiri wao pekee ni kwa mguu, au kupanda punda. Nao walikuwa hapa pamoja na punda mdogo anayetembea pole pole; na tunaweza kutembea zaidi yake. Na yeye alikuwa hapa, safari ya siku tatu, na ndipo akainua kichwa chake na akauona mlima kwa mbali bado. Lazima yeye alikuwa kama maili mia mbali na ustaarabu nyuma kule jangwani. Sasa sikilizeni na mwone.

63 Ndipo yeye akachukua zile kuni na kuziweka mgongoni mwa Isaka; msalaba, Mwana wa Mungu miaka kadha baadaye. Na Isaka alibeba zile kuni hadi juu ya kilima,

kile yeye alichokuwa anakwenda kulala juu yake kwa ajili ya dhabihu. Kutangulia kwa kivuli.

Kama Mungu alitanguliza kivuli cha hilo hadi kufuatilia kwa makini; mke wa Lutu, je usigeuke na kutazama nyuma kuelekea mambo ya ulimwengu. Mifano hiyo yote na vivuli ni vikamilifu. Unaona? Mkumbukeni Hawa. Mkumbukeni mke wa Lutu. Mkumbukeni Lutu mwenyewe, wewe mwanamume. Kumbukeni, Adamu alijitolea kwa mke wake; Lutu, vivyo hivyo. Uwe mwangalifu. Mimi nawaambia tu, kama ndugu. Muda umeendelea kuliko unavyofikiri.

Mtazame Isaka mdogo akikwea kilima. Naye akapata mashaka. Na yeye akatazama huko na huko, akasema, "Baba yangu?"

Naye akasema, "Mimi hapa, mwanangu."

Isaka akasema, "Hapa kuna kuni. Na hapa kuna vyote, kila kitu, moto. Lakini yuko wapi kondoo wa sadaka ya kuteketeza?"

Msikilize yule baba mzee, pasipo na kutetemeka katika sauti yake, yeye alisema, "Mwanangu, Mungu atajipatia Mwenyewe hiyo dhabihu." Mwanawe pekee akienda kwenye machinjio, lakini bado ule moyo mwaminifu wa kale ulikuwa umejua kuwa Mungu hawezi kusema uongo…

Huo ndio Uzao wa Abrahamu leo! "Inawezekanaje, Ndugu Branham?" Mungu atajipatia Mwenyewe! "Yeye atafanyaje?" Mimi sijui. Lakini Yeye ni Yehova-Yire!

64 Akafika kwenye kilele cha kilima, wakiliviringisha lile jiwe hadi juu. Akaweka kuni juu ya yale mawe, na kuziwasha hizo moto. Akasema, "Isaka, mwanangu, geukia kule." Akachukua kamba kuizingira kiunoni mwake, na kumfunga mikono yake na miguu yake. Isaka, akiwa mtiifu, kama Kristo alivyokuwa, hadi mauti. Akamlaza pale juu ya pande la jiwe. Akaingiza mkono wake kufikilia katika ala na kuvuta kisu kikubwa; akakinoa kwa mara kadha, akiwa anatazama kuelekea angani.

"Yeye hakuyumba penye ahadi ya Mungu kwa kutokuamini, bali alikuwa imara, akijua kwamba yeye alikuwa amempokea mtoto akiwa kama aliyetoka kwa wafu; alishawishika kikamilifu kuwa kama Mungu alisema hivyo, kuwa yeye afanye hilo, Yeye Mungu angeweza kumfufua kutoka kwa wafu." Huyo ni Abrahamu, na huo ni Uzao wake baada yake. Kama huo ulikuwa uzao wa asili, ule Uzao wa kifalme unapaswa uweje? Hakuna kuyumba! Kile Mungu alichosema, Mungu atakifanya. Akijua hilo, yeye alishawishika kikamilifu; kwamba kile Mungu alichokwishaahidi, Mungu alikuwa anaweza kufanya.

65 Alinoa kisu; macho madogo meusi ya Isaka mdogo yakiwa yanatazama ubapa mkali wa kisu kilipokuwa kinanolewa juu ya lile jiwe. Akarudi nyuma; akarudisha nyuma nywele zilizokunjamana kutoka usoni pake, akavuta nyuma kidevu chake kidogo. Akainuka, na machozi yakiwa yanatiririka usoni mwake namna ile. Akijua, na yeye hakuyumba penye ile ahadi ya Mungu! Akainua kichwa chake ili kuzamisha kile kisu katika koo la mwana wake mwenyewe.

Naye alipofanya hivyo, sauti ya Mungu iliita, na kumshika mkono wake, ikasema, "Abrahamu! Abrahamu, zuia mkono wako! Sasa najua kwamba unanipenda." Yeye Bwana alikuwa anafanya nini? Akitoa ushuhuda kwa Uzao wa Abrahamu, baada yake. "Zuia mkono wako, usimdhuru huyu mtoto! Najua kuwa unanipenda."

66 Na karibu wakati ule, Abrahamu alisikia kitu fulani nyuma yake. Naye akatazama, na kulikuweko na kondoo dume (huyo ni kondoo dume) aliyenaswa pembe zake katika magugu na vichaka. Na Abrahamu akaenda na kumchukua yule kondoo dume na kumwua, badala ya mwanawe.

Yule kondoo dume alitokea wapi? Yeye yuko maili mamia mbali na ustaarabu. Mbona, wanyama pori wangeliweza kumwua kama yeye angelikuwa nyuma kule. Hakika, yeye ni-yeye ni mnyama wa kufugwa. Yeye alitokea wapi? Na, mbali na hilo, ni mbali kule juu ya mlima, kule ambako hakuna majani wala maji. Na Abrahamu aliokota mawe kote huko, pale huyo kondoo dume alikokuwa, ili kutengeneza madhabahu. Yeye alitokea wapi? Hilo halikuwa ono; yeye alitokwa na damu. Ono huwa halitokwi na damu. Haleluya! Yehova-Yire alikuwa amejipatia dhabihu Mwenyewe.

67 Mungu anapochukuliwa kwenye Neno Lake, Yeye anaweza kutoa chochote kile anachotaka. Mungu, Yehova-Yire, bado ni Yehova-Yire jioni hii! Yeye amekwishajipatia

Dhabihu. Yeye amekwishajipatia Kanisa. Yeye amekwishajipatia Mjumbe, Roho Mtakatifu. Yeye yupo hapa sasa, Yehova-Yire! Bwana amejipatia Mwenyewe Biblia, Roho, Ujumbe, Mjumbe. Na ile saa iko hapa sasa kwa ajili ya kunyakuliwa kwa Kanisa na kupelekwa nyumbani. Yehova-Yire atatoa njia ya kuliondoa hilo Kanisa kutoka kwenye huu ulimwengu, kwa kubadilishwa kutoka kwenye hii miili yetu iliyo midhaifu, na kuipeleka juu Utukufuni. Yehova-Yire! Hilo litatukia vipi katika siku ya kisasa kama tunayoishi, kuwa haya mambo yatatokea.

68 Billy, mwanangu, popote alipo, na mimi, tulikuwa India hivi karibuni tu. Nilichukua gazeti…Nilipotoka kwenye meli, maelfu walikuwa wamesimama pale pamoja na malundo ya mashada. Tulipofika kule kwenye Taj Motel, wao walikuwa na gazeti likiwa limekaa pale, katika Kiingereza. Na niliona kipande kikubwa ndani yake, kilichosema, "Hiyo ni lazima iwe ishara kuwa tetemeko limekwisha." Tatizo lilikuwa nini? Vema, kama siku tatu au nne hapo kabla lile tetemeko kuu mlilosoma juu yake, ndege wadogo wote walioishi katika miamba…

Katika India, wao hawana kuta nyuzio tulizo nazo katika California, Amerika. Wao hutengeneza nyuzio kutokana na mawe wanayoyaokota. Na hao ndege wadogo hujenga kiota chao ndani yake. Wao hujenga minara mikubwa, na ndege hujenga viota vyao ndani yake. Na hao ndege wadogo wote, siku kadhaa hapo kabla ya tetemeko kuja, waliruka na kuondoka kutoka kwenye hizo kuta. Na wakati wa jioni au…Katikati ya mchana, wakati kulipokuwa na joto, kondoo na ng'ombe wangesimama chini ya kivuli cha ukuta na mnara, ili kujikinga na jua kali.

Lakini kwa siku mbili, ng'ombe na kondoo kamwe hawakuja katika kuta. Wao walisimama nje katikati ya shamba na kuegemeana wao kwa wao, kwa ajili ya faraja. Ndipo tetemeko likaja, likaangusha chini hizo kuta. Na ndipo hao ndege wadogo wakaanza kurejea, ng'ombe kutoka mashambani. Ilikuwa ni kitu gani? Mungu yule yule aliweza kuwaita hao kondoo na ng'ombe, na ndege, waingie katika safina, alionyesha kuwa Yeye ni Mungu yule yule leo anayeweza kuwaita wanyama Wake waondoke.

69 Na kama Yeye anaweza kumwongoza mnyama kwa njia ya hisia za silika, ni kiasi gani zaidi Kanisa la Mungu linapaswa kuondokana na hizi kuta kubwa zilizoundwa na mwanadamu na mafundisho ya makanisa. Babeli itaanguka, baadhi ya hizi siku. Yehova-Yire amejipatia Mwenyewe Mahali pa Pumziko kwa ajili yenu. Rukeni muondoke kwenye minara ya ulimwengu!

Ondokeni kwenye mvuto sana wa Hollywood! Makanisa yanawadhihaki, kung'ara. Injili haing'ari. Hollywood inang'ara, Injili inawaka. Hollywood inang'ara kwa mvuto sana. Kanisa kubwa linang'ara kwa elimu. Na Kanisa la Mungu aliye hai linawaka kwa unyenyekevu na uzuri, na Roho Mtakatifu. Kuna tofauti nyingi kati ya kuwaka na kung'ara.

70 Yeye yupo hapa sasa. Yehova-Yire amejipatia Mwenyewe. "Mungu anaweza kumwinulia Abrahamu watoto kutokana na haya mawe." Kama madhehebu hayawezi kukubali Hilo, Mungu anaweza kuleta watoto Wake kutoka mabarabarani, makahaba kutoka kwenye nyumba za kulala wageni. Yeye anaweza kuinua kitu chochote anachotaka kuinua. Lakini kama Mungu amejipatia Ujumbe, kuna mtu fulani mahali fulani wa kuupokea Huo. Yehova-Yire! Bwana atajipatia Mwenyewe Ujumbe. Bwana atajipatia Mwenyewe Mjumbe. Bwana atajipatia Mwenyewe, katika njia Yake Mwenyewe, hizo ishara kwa Kanisa; siyo kujiunga, kuweka majina kwenye vitabu.

Tunasikia mengi mno leo juu ya kukata shauri, kukata shauri kwingi mno. Kuna manufaa gani kulundika mawe kama huna fundi mwashi pale ili kuikata na kuchukua maumbo kuwa wana na mabinti wa Mungu? Ina faida gani kujenga madhehebu makubwa kwa maelfu, kama kuna mtu fulani hayupo pale akiwa na Upanga wa Mungu wenye makali pande mbili ili kuwaunda hao kuchukua maumbo kuwa watoto halisi wa Mungu? Unaweza pia kuwaacha hapo walipo. Amina. Mungu (siyo Methodisti, siyo Baptisti, Katoliki), Mungu amejipatia Mwenyewe Kisu ili kuwaunda kuchukua maumbo watoto wa Mungu, wana wa Mungu. Amina. Yehova-Yire, "Bwana atajipatia Mwenyewe." Na Yeye amejipatia! Mwamini Yeye, na uishi.

71 Hebu tuinamishe vichwa vyetu kwa kitambo kidogo.

Mungu mwenye neema, Mungu aishiye milele na milele, uturehemu sasa, na utupe neema Yako. Sisi hatustahili, Baba, kwa kitu chochote ambacho Wewe ungetutendea. Lakini hatukiri kuwa tunastahili, bali tunatii tu wito kutoka kwa Mungu. Tunaomba, Baba,

kwamba utatuunda kuchukua maumbo jioni hii kuwa mawe yatakayofaa katika Hekalu la Mungu, kwa ajili ya Kuja kuliko kukuu kwa Bwana Yesu Hekaluni Mwake. Tujalie hilo, Baba. Tusamehe mapungufu yetu sisi wenye dhambi. Tufunulie Neno Lako. Tuonyeshe njia ya kutembea. Tufundishe. Ewe Baba, Mungu. Hebu sisi tulipokee Hilo. Na kama hilo ni kinyume na Neno, tunajua kuwa ni mwalimu aliye makosani. Roho Mtakatifu ndiye mwalimu wetu. Yeye aliliandika Neno, na Yeye asingelifundisha kitu chochote isipokuwa Neno. Nasi tunaomba kuwa Yeye atalidhihirisha Hilo kwetu jioni hii, katika moyo wetu. Tujalie hilo, Mungu.

72 Sasa tukiwa tumeinamisha vichwa vyetu, macho yetu yakiwa yamefumbwa. Neema ya Mungu hukaa juu ya hili, ni maombi yangu ya unyenyekevu na uaminifu. Amini tu sasa. Usitie shaka.

Je, kuna mtu yeyote ndani ya jengo, ambao najua wapo, wanaume na wanawake ambao hawamjui Yeye, hawajawahi kamwe kuikubali Dhabihu Yake aliyojipatia, Bwana Yesu, kama Mwokozi wako? Je, wewe humjui Yeye? Huenda ukawaza kiakili kuwa unamjua. Lakini mtu hawezi kumwona Mungu hadi yeye azaliwe upya. Unaona halimaanishi…Huoni kwa macho yako; unatazama kwa macho yako. Kuona ni "kuelewa." Ulilitazama hilo kwa usahihi, na kusema, "Mimi sioni hilo," unamaanisha "wewe hulielewi hilo." Kamwe hutajua kile tunachokizungumzia hadi uzaliwe upya. Kamwe hutakuwa na huo uzoefu? Mkiwa mmeinamisha vichwa vyenu sasa, na macho yenu yakiwa yamefumbwa, je ungeinua mkono wako, na useme, "Ndugu Branham, nikumbuke katika maombi jioni hii. Naamini kuwa tunapokea Ujumbe wetu wa mwisho. Ile siku inaponyoka kwa kasi. Na naona kuwa kile ulichosema katika Biblia ni ukweli kwa sababu nimesoma Biblia. Naamini kuwa ni saa ambayo ni lazima tuje sasa. Na, kwangu mimi, naweka msimamo wangu sasa kwa ajili ya Kristo."

73 Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki, wewe. Vizuri. Juu katika roshani, hiyo mikono! Inua tu juu mkono wako, useme, "Mimi, kama Yoshua alivyosema, 'Mimi na nyumba yangu, tutamtumikia Bwana.'" Vema, mtu fulani mwingine? Nasubiri tu. Mungu akubariki nyuma kule. Naona mkono wako. Mungu akubariki juu kule. Mungu akubariki. Yeye anakuona. Juu kule katikati roshani, Mungu akubariki juu kule, bwana; kitu kikuu zaidi ya vyote ulichowahi kufanya katika maisha yako. Pale pale katikati ya njia ya safu za viti, mtu fulani aliinua juu mkono wake pale. Labda sikuwahi kamwe kuona mkono ndani pale, huenda…Mtu fulani katika hii njia kati ya safu za viti iliyo katikati, kuna wowote ulioinuliwa juu? Inua juu mkono wako, na useme, "Ndugu Branham, mimi, nina…Nataka kumtumikia Yeye. Mimi-mimi ni mwaminifu." Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki mwanamume mdogo. Katika roshani upande wa kuume, watu fulani wainue mkono wao, waseme, "Ndugu Branham, mimi, kwangu mimi, najua hilo ni sahihi. Nina-simjui Mungu, lakini nataka nimjue Yeye. Nataka niwe na hakika. Naona siwezi kubahatisha. Kamwe sitarudi tena."

74 "Mti unakoegemea ndiko unakoangukia," Andiko linasema. Usiangukie upande ulio wa makosa. Unaweza kufanya hilo kuwa sahihi jioni hii. Kumbuka, maadam kuna Umilele, na kamwe huo haukuwa na mwanzo na kamwe hautakuwa na mwisho, bali wewe unafanyika kuwa sehemu yake, utateseka au utaishi katika furaha. Unajuaje kama utaishi hadi ufike nyumbani?

Unasema, "Mimi ni kijana mno."

Nilipata tu ujumbe kitambo kidogo kilichopita. Bibiye kijana nyuma katika jimbo langu, aligeukia tu njia za makosa, akaanza kuvuta sigara. Yeye alikuwa ameambiwa juu ya Mungu, lakini hakusikiliza. Akiwa na umri wa miaka kumi na sita, yeye alikuwa anatokea…hapana, umri wa miaka kumi na nane, ndiyo tu amerejea kutoka sekondari ya elimu ya juu. Naye aliambiwa, akijaribu kufanya lililo sahihi. Lakini alianza kuambatana na kundi la makosa, radi ilimwua papo hapo.

75 Hivi karibuni tu, mwanamume mweusi katika Shreveport alisimama na kusema, "Hakuna kitu kama Mungu." Alikufuru tu, akasema, "Hao si kitu chochote bali kundi la watakatifu wanaojiviringisha." Radi ilimwua yeye. Wakampeleka kaburini. Na walipokuwa wanamzika huyo mwanaume, wingu dogo likajitokeza, na radi ikalipiga lile jeneza na kumlipua na kumtoa nje ya hilo jeneza.

Yehova Mungu hukasirika. Najua Yeye ni Mungu mwema, lakini Yeye ni Mungu wa hukumu, pia. Yeye bado anatazama, Yeye anajua.

Kama wewe huna Mungu, inua juu mkono wako, useme, "Nikumbuke, Ndugu Branham, unapoomba." Mungu akubariki, bibiye. Mungu akubariki, mwana. Hilo ni sahihi, njoo moja kwa moja mbele. Mungu akubariki. Hilo ni sahihi, kijana. Mungu akubariki nyuma kule. Ndiyo nyote nyuma...?...

76 Baba yetu wa Mbinguni, sasa Wewe unawaona hao. Wewe unajua kuna mikono ishirini au thelathini iliyoinuliwa juu, ambao wanakuhitaji Wewe kwa ajili ya Mwokozi wao, Mungu, tujalie hili sasa hivi. Nawapa wao hili Neno. Ulisema Mwenyewe, "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu." Mimi nimefanya kadiri niwezavyo pamoja na Hilo, Bwana. "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu na kumwamini Yeye aliyenituma, anao Uzima wa Milele, naye hataingia hukumuni, bali amekwishakupita kutoka mautini kuingia Uzimani." Ni kitu kizuri iliyoje, kuwazia hilo! Kama mioyo minyoofu iliyo nyuma ya hiyo mikono, inamaanisha hilo hasa, jambo fulani limetukia tu. Sasa Wewe ulisema, "Yeye atakayenikiri mbele za wanadamu, nami nitamkiri mbele za Baba Yangu na Malaika watakatifu. Hebu wao wajue kuwa Wewe uko hapa, Bwana. Naomba kwamba utatujalia hilo. Tusikie. Sisi ni watumishi Wako, Bwana. Katika Jina la Yesu.

77 Vema, inua kichwa chako. Je, mnaamini Yeye ni Yehova-Yire? [Kusanyiko linasema, "Amina."-Mh.] Je, mnaamini tuko katika siku kama ilivyokuwa katika siku za Lutu? ["Amina."] Siku za Nuhu? ["Amina."] Mnakumbuka ule Ujumbe wa mwisho?

Je, kuna mtu fulani hapa kwa mara yao ya kwanza? Inua juu mkono wako. Wengi! Nadhani Ndugu Borders amewaelezea kwetu. Mmesikia juu yangu hapo kabla, hilo lililotukia. Inueni mikono yenu juu, kama uliwahi kusikia; kama hukuwahi kamwe kuona hilo, umelisikia tu. Vema. Sasa mimi ni mgeni kwa watu hapa.

78 Baadhi yenu watu wenye tatizo, ombeni Mungu, na mseme, "Mungu, unirehemu, mimi ni mgonjwa. Ndugu Branham hanijui. Lakini nasikia kuwa Wewe ni Kuhani Mkuu awezaye kuguswa na hisia za madhaifu yetu." Ni wangapi wanajua hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."-Mh.] "Na Yeye ni yule jana, leo, na hata milele na milele." Je, mnajua hilo? ["Amina."] Vema, sasa, kama Yeye ni yule yule Kuhani Mkuu, Yeye angetendaje kama ulimgusa Yeye? Jinsi ile ile Yeye alivyotenda wakati yule mwanamke mwenye jambo la damu alivyomgusa Yeye. Yeye aligeuka na kumwambia ile hali yako ya damu ilikuwa nini, na kumwambia imani yake imemwokoa. Je, hilo ni sahihi? Yeye ni Yule Yule jioni hii, kama unaweza kumwamini Yeye kwa namna ile ile aliyokuwa nayo wakati ule. Je, mnamwamini Yeye namna hiyo?

Sasa tazameni upande huu, kwangu. Kama Petro na Yohana walivyosema pale penye Lango Zuri, "Tutazame," Hilo halikuwa "Watazame wao," kwa ajili ya lolote, bali, "tazama kile wao walichokuwa wanasema."

79 Hebu tuanzie hapa mahali fulani. Tazameni upande huu, na amini kwa moyo wako wote. Na useme, "Bwana Yesu, nakuamini, na nataka kugusa vazi Lako. Unene na Ndugu Branham, na umruhusu yeye ajue tatizo langu ni nini. Nitakuamini kama utafanya hilo." Je, ungefanya hilo?

Sasa hapa kuna kile kitu hasa. Je, mimi ningethubutu kufanya kitu kama hicho? Ningekuwa na kitu fulani cha makosa kufanya makabiliano namna hiyo. Nimekabiliana na hilo mbele ya watu nusu milioni, kwa wakati mmoja, sikuweza hata kunena lugha yao. Lakini Yeye hakuniacha kamwe. Kwa nini? Yeye aliahidi hilo! Hizi ni siku za mwisho, na Yeye aliahidi hili, na ndilo hili hapa.

80 Najua, marafiki, mmekuwa na wengi wa kuwaumiza. Mmekuwa na uigizaji mwingi wa kimwili. Lakini hebu niseme jambo moja kwenu, siyo kwa faida yangu, bali kwa faida yenu wenyewe. Wao wamekuwa nacho daima. Mungu kamwe hajawa na wawili duniani kwa wakati mmoja, kamwe hakufanya. Lakini kumbukeni tu, kuna uigizaji mwingi, lakini yuko Mungu halisi. Kuna Roho Mtakatifu halisi. Kuna Ujumbe halisi wa Mungu, na hilo ni kwamba Yesu Kristo alikufa kwa ajili ya wenye dhambi, akafufuka tena kutoka kwa wafu, naye akarejea katika Utu wa Roho Mtakatifu, ili atende matendo yale yale katika Kanisa yale aliyotenda alipokuwa hapa.

81 Sasa, je, Neno la Mungu halisemi hili? Katika Waebrania, lilisema, ile sura ya 4, Biblia ilisema kwamba, "Neno la Mungu ni kali, lina nguvu zaidi kuliko upanga wenye makali pande mbili, likitenganisha," hiyo ni kukata kuwili kuja na kuondoka, "na hata kwenye mafuta ya mfupa, na Mtambuzi wa mawazo na makusudio ya moyo." Je, hilo ni sahihi?

Hiyo ndiyo sababu Yesu aliweza kusimama mbele ya hadhara na kuwaambia. Hao Mafarisayo walisema, "Yeye ni Beelzebuli." Yesu aligeuka. Wao hawakunena hilo kwa sauti ya juu, lakini Yeye aliwaambia. Hiyo ndiyo sababu Yeye aliweza kumwambia yule mwanamke juu ya lile jambo la damu. Alimwambia yule mwanamke yeye alikuwa na waume , na yeye alipofanya hivyo, Bwana alisema, "Mbona, hiyo ni ishara ya Masihi."

Unaona sasa kurejea , kutokea kwa Masihi miongoni mwa watu. Ni Roho Mtakatifu akiliandaa Kanisa kuwa tayari.

82 Nataka ugeuze kichwa chako. Mnamwona yule mwanamke anayefikia pale, akiinua mgongo juu, akiketi hapa hapa chini? Je, mnaona hiyo Nuru juu yake? Yeye anaumwa na shinikizo la juu la damu. Hilo ni sahihi. Amevaa gauni la rangi ya samawi, namna ya kuvaa miwani usoni mwake. Kwa sekunde moja iliyopita au mbili, alikuwa anajisikia hali ya joto kwa ajabu hasa kumzunguka. Hilo ni sahihi. Sasa shinikizo lako la damu, ambalo limekuwa llikikusumbua vibaya mno, limekutoka. Unalikubali hilo? Inua juu mkono wako kama unalikubali.

Yeye aligusa nini? Kuhani Mkuu. Sasa nenda, umwulize huyo bibiye. Kamwe sikuwahi kumwona katika maisha yangu. Sijui jambo hata moja juu ya huyo mwanamke; lakini, huo ni ukweli. Nilikuwa nikiitazama hiyo Nuru ilipokuwa ikitembea kukatisha hii hadhara, ilikwenda moja kwa moja pale na kurudi, Nuru inayowaka.

83 Je unaamini? Baridi kavu, tatizo la kibofu, magonjwa ziada, wasiwasi, udhaifu. Hilo ni sahihi. Wewe hutokei hapa. Sehemu ndogo iitwayo West Point. Hilo ni sahihi. Je, unaamini Mungu anaweza kuniambia wewe ni nani? Bi Hardwick. Hilo ni sahihi. Kama hilo ni sahihi, simama juu kwa miguu yako. Huo umekuacha. Yesu Kristo anakufanya kuwa mzima.

Je, mnaamini? [Kusanyiko linasema, "Ndiyo."-Mh.] Watu wanaangalia kuelekea nyuma, kwa ajili yake. Hapa ameketi huyo bibiye papa hapa. Tazama, Hiyo Nuru bado iko juu yake. Je, hamuioni Hiyo? Hapa Hiyo hapo. Tazama?

Hiyo iko pale, na yule mwanamume aliyeketi pale pale akinitazama. Baridi kavu. Amini kwa moyo wako wote, Mungu atakufanya kuwa mzima, bwana, pia. Sisi ni wageni mmoja kwa mwingine, lakini siyo kwa Mungu.

84 Huyu bibiye hapa hapa nyuma hapa, anaumwa na kichwa. Mungu, usimwache alikose hilo. Ewe Mungu, tafadhali. Bi Morton, mwamini Bwana Yesu Kristo. Yeye alikuponya hicho kichwa. Unaona, Yeye hangeruhusu limpite yeye. Nataka kuwahitaji jambo fulani. Usiku wa jana niliponena na mtu fulani ndani ya jengo hili juu ya kuumwa kwao kichwa, ulikuwa na kujisikia kusiko kwa kawaida, na ulikuwa unajiuliza kama hilo lilikuwa wewe, au la. Je, hilo ni sahihi? Inua juu mkono wako. Mimi sisomi akili zako, bali nakuambia kile ulichokuwa ukifikiri. Hilo ni sahihi. Leo Yeye alitaka kuwa na hakika kuwa ilikuwa ni wewe. Hilo litaondoka kwako sasa, imani yako imekuokoa. Haleluya.

85 Mtazame huyu bibiye aliyeketi hapa, aliyevaa gauni la mirabamiraba ya rangi mbalimbali. Je, unayo kadi ya maombi, bibiye? Tazama ya kwako mwenyewe. Je, unaamini ugonjwa wa ngiri utakuacha, utakuwa mzima? Unaamini? Inua juu mkono wako kama hilo ndilo tatizo lako. Vema. Amini kwa moyo wako wote na uponywe. Unaona unalotaka?

Yule bibiye pale pale nyuma yake, aliyeinua juu mkono wake, akiwa na dogo…hapana, wa pili nyuma pale, aliyevaa gauni linaloonekana kuwa la rangi ya kijani, akiwa anaumwa na ugonjwa wa moyo. Ndiyo. Je, unaamini kuwa Mungu atakufanya kuwa mzima? Hilo ni zuri, mtu maridadi. Yeye atakufanya kama utaamini hilo.

Bibiye, wa pili pale kutoka kwako, Bibi Dillman pale. Kama unaamini kuwa Mungu atakuponya hilo tatizo la tumbo. Bibi Dillman, amini, na utakuwa na tumbo lako. Ni kuvurugika kwa tumbo, limekuwa nawe kwa muda mrefu, hasa limekuwa nawe tangu ufikie ukomo wa hali ya kike. Umekuwa na mambo mengi ya kukusababishia shida, lakini hilo lote limekwisha sasa. Kama hayo mambo ni kweli, pungia tu watu mkono wako, ili kwamba waweze kuona. Kama mimi ni mgeni kwako, endelea kupungia mkono wako. Yesu Kristo amekufanya kuwa mzima.

86 Je, mnaamini? [Kusanyiko linasema, "Amina."-Mh.] Hicho ni kitu gani? Yehova-Yire, Bwana anajipatia Dhabihu Mwenyewe! Sasa kusanyiko lote linakuwa kama limekuwa na ukungu kwangu. Yehova-Yire amejipatia Dhabihu kwa ajili ya kila mmoja wenu. Je, mnaamini hilo?

Sasa wewe, uliyeinua mkono wako juu hapa, njoo juu hapa na usimame hapa kwa muda mfupi. Je, utafanya hilo? Yehova-Yire amejipatia Dhabihu. Uliinua juu mkono wako, kwamba unaamini hilo. Umeona hapa, na kujua. Haiwezekani…Ni Kitu fulani! Tazama hawa watu, ni wangapi walioitwa. Mimi sijui. Labda saba, nane au kumi, chochote kile, walioitwa. Hilo linaweza tu kuwa linaendelea. Lakini niwapo na nguvu, nataka uje umkubali Kristo kama Mwokozi wako. Ungeinuka sasa na kuja, hali tunapoimba. "Nakuja, Bwana, nakuja Kwako sasa"? Je, utainuka sasa na uje juu hapa, wewe uliyeinua juu mkono wako kitambo kidogo kilichopita? Na usimame hapa madhabahuni, na uonyeshe kuwa humwonei haya Kristo. Uko Uweponi Mwake. Njoo sasa, na uthibitishie watu kuwa ulimaanisha hilo hasa, kwamba unataka kukumbukwa na Mungu, nawe umemkubali Yeye kama Mwokozi wako. Njoo juu sasa, sote tunaposimama na kuimba.

> Nakuja, Bwana!
> Sasa nakuja Kwako!
> Nioshe, nitakase katika Damu
> Iliyotiririka kutoka Kalvari!

Toka sasa, njoo moja kwa moja chini hapa. Tunakwenda kuomba. Kamwe hutakuwa karibu zaidi na Yeye utakapo…?....

> Sasa nakuja Kwako!
> Nioshe, nitakase!

87 Shuka chini moja kwa moja kutoka roshani. Naam, shuka chini moja kwa moja, simama papa hapa. Yeye ata … Sasa Yeye alisema, "Kama utanikiri Mimi mbele za watu, nami nitamkiri yeye mbele za Baba Yangu. Lakini kama unanionea Mimi aibu, nami nitakuonea aibu," kumbuka, Biblia, toka Mwanzo hadi kwenye Ufunuo. Njoo sasa, kijana na mzee. Je, utakuja? Mshirika wa kanisa, au la, njoo sasa. Utakuja? Mkubali Kristo unapokuwa katika Uwepo Wake.

> Nakuja, Bwana!
> Sasa nakuja Kwako!
> Nioshe, nitakase katika Damu
> Iliyotiririka kutoka Kalvari!

(Hebu endelea tu kuwaongoza.)

88 Sikilizeni. Je, mnaniamini mimi kuwa nabii Wake? Sijakiri hilo hapo kabla. Lakini naamini, kwa kusema hilo, watu wataelewa na kujua kile ninachojaribu kukiendea. Kuna watu ndani hapa wanaoukiri Ukristo, wangelikuwepo hapa. Njoo, hutakuja? Hebu nikuhitaji, wewe unakwendaje? Kamwe hutapokea ishara nyingine. Ndiyo hii. HIVI ASEMA BWANA. Je, nabii wa Mungu angetoa tamshi kama hilo kama halikuwa ukweli? Unapokea ishara yako kuu zaidi ya zote, na ishara yako ya mwisho, kabla ya kutokea kwa Kristo. Njoo! Sababu ninasema haya mambo, kamwe sijasema hili katika mkutano mwingine wowote, najisikia kuwa hapa hapa ndiyo nafasi hapa kwa kutukia jambo fulani. Na hiyo ndiyo sababu mimi ninasema namna hii. Naamini mtaelewa. Usingekwenda huko na huko, ufanye namna ya madhehebu, useme, :Ndugu Branham ni mungu,‟ au kitu fulani kama hicho. Mnaelewa kile ninachokizungumzia. Njoo sasa. Njoo. Hebu nikushawishi, katika Jina la Kristo. Njoo!

89 Wewe usiyejua pale ulikosimama, huna hakika juu ya hilo, ni ya kiakili tu, au aina fulani ya msisimko; umepiga yowe, umelia, au wewe-wewe umekuwa na namna fulani ya hisia. Usijaribu kuingia ndani juu ya hilo. Kumbuka, nakuambia katika Jina la Bwana, kuwa umepotea, umepotea katika hali ya huzuni, nawe hujui hilo. Usibahatishe, rafiki. Mimi napanda tu mbegu, na kuvuta wavu. Mungu huchukua kuongeza. Mimi sijui.

Hebu tuinamishe vichwa vyetu, tuone kama Yeye kama hataniambia mimi. [Dada fulani ananena kwa lugha nyingine, na ndipo anafasiri-Mh.] Mnasikia hilo.

> Nakuja sasa Kwako! (Uchunguze moyo wako)
> Nioshe, nitakase katika…

90 Mshirika wa kanisa. Kama mimi nilikuwa nimesimama pale, na niwe tu na uzoefu wa kujiunga na kanisa mahali fulani, ningekuja hapa kwa haraka tu niwezavyo.

Kumbukeni, Roho akishuhudia kuwa tuko mwishoni. Sayansi ilisema, "Bado dakika tatu ifike usiku wa manane." Ujumbe na Biblia vinasema, "Ndicho hiki hapa, kile kitu cha

mwisho!" Uamsho unaishia, mlango unafunga. Wewe utakuwa upande wa nje, ukibisha hodi, na hutaweza kuingia ndani. Njoo!

Mungu akubariki, bibiye kijana.

Na [neno lisiloeleweka] fanya hilo

Nakuja, Bwana!
Sasa nakuja…

Mungu akubariki. Hilo ni sawa, bwana. Hiyo ndiyo njia, shuka chini moja kwa moja kutoka roshani. Ukija kupitia hizo safu.

91 Hapa kuna Neno, hapa kuna ushuhuda. Pale yuko Roho, pale kuna shahidi. Na hapa watu wanakuja, ili kuonyesha kuwa tuko hapa penye wakati wa mwisho.

Nakuja, Bwana!
Sasa nakuja Kwako!
Nioshe, nitakase katika Damu
Inayotiririka kutoka Kalvari!

Nakuja, Bwana!

Akisubiri, akivumilia, hapendi yeyote apotee bali wote waweze kuja kwenye toba. Njooni, simameni hapa.

Kama umekuwa na shaka akili yako. Inakupasa uwe na hakika, marafiki, imani ni kamilifu.

… kutoka Kalvari!
… Bwana!
Sasa nakuja kwenye…

Njooni. Kiasi cha watu hamsini, sabini waliokusanyika hapo. Sasa njoo. Hebu hao wengine ambao watakuja. Tukiendelea zaidi kidogo sasa. Kwa sababu, kesho itakuwa juu ya uponyaji wa Kiungu. Roho Mtakatifu aliniambia, kitambo kidogo kilichopita, "Usiite huo msitari. Ita madhabahuni." Natamtii Yeye, nafanya anavyoniambia Yeye. Namtii, Yeye inampasa afanye jambo hilo.

Sasa nakuja Kwako!
Nioshe, nitakase katika Damu
Iliyotiririka kutoka Kalvari!

92 Vichwa vyetu vikiwa vimeinamishwa sasa, tunaposubiri. Ewe Mungu, hebu Roho Mtakatifu atembee ndani juu ya hawa. Hao wanaotaka kuja mbele madhabahuni, akiongoza watu sasa kwenye baraka. Na hebu Bwana atujalie jambo hilo. Roho wa Mungu, akinena.

Ingia ndani, ingia ndani. Njoo karibu sasa, kila mmoja. "Kila nafsi, iliyokandamizwa na dhambi, Kuna rehema kwa Bwana." Njoo sasa, "Njoo chini ya mafuriko yatakasayo, Yanayoondoa madoa yote ya makosa yao. Kuna Chemchemi iliyojaa Damu, Kutoka kwenye mishipa ya Imanueli. Kwa unyenyekevu.

93 Je, unahisi hiyo amani juu ya mkutano sasa? Ni kitu gani? Ni kifo, kifo kwa wenye dhambi. Sasa wafanyakazi binafsi ingieni hapa pamoja nao sasa. Ni kifo, hawa watu wanakufa. Biblia ziko nje, zinaelezea. Kifo kinaenda huko na huko madhabahuni, na Uzima mpya utakuja baada ya kifo.

Kuna Chemchemi iliyojaa Damu,
Iliyotekwa kutoka… (Ee, ungependa iliyoje
kusikia hilo siku fulani, ile siku mapigo ya moyo
wako yatakapokoma.)
Na wenye dhambi kutumbukizwa chini ya hayo
mafuriko,
Madoa yao yote ya dhambi yakaondolewa.
Madoa yao yote ya dhambi yakaondolewa.
(Ndilo hilo, jamaa kijana. Moyo wako
ubarikiwe. Hilo ndilo Yeye alilokuwa analisubiri.)
Na wenye dhambi kutumbukizwa chini ya hayo

mafuriko,
Madoa yao yote ya dhambi yakaondolewa.

94 Sasa hebu Wakristo ambao wameelekezwa, watembee kuja juu tunapoimba ile aya inayofuata. "Yule mwizi aliyekuwa anakufa alishangilia kuona ile Chemchemi katika siku yake; huenda mimi, ijapokuwa mwovu kama yeye, nioshe dhambi zangu zote." Hebu hao watu wanaoelekeza sasa watembee kuja juu kwa karibu. Ninyi ambao hamna ubatizo wa Roho Mtakatifu, tembeeni kuja juu karibu sasa. Hamjui kile Mungu anaweza kufanya sasa katika muda mfupi. Tembeeni kuja juu sasa, tunapoimba aya inayofuata sasa.

Yule mwizi aliyekuwa anakufa alishangilia…
(Neno lilidhihirika) Chemchemi katika siku yake;
(Ee, hilo ni zuri, tembea utoke moja kwa moja
sasa. Njoo wakati Maji yamevurugwa)
… ni mwovu kama yeye,
Nioshe dhambi zangu zote.
Nioshe dhambi zangu zote,
Nioshe dhambi zangu zote;

Sasa, ndilo jambo lenyewe, wafanyakazi. Njooni moja kwa moja ndani, nyote…?... sasa, kwa ajili ya Maji kuvurugwa. Njooni juu moja kwa moja.

… mwovu kama yeye,
Nioshe dhambi zangu zote.

95 Sasa ninyi mnaotaka kuomba, tembeeni kuja juu kwa karibu sasa na mmwe tayari. Tunakwenda kuamini kuwa Mungu atalitambua hili. Inampasa Yeye alitambue! Mungu yule yule anayeweza kutambua wazo la moyo! Kumbukeni, Yesu alifanya hilo wakati mmoja katika mji. Lakini Yeye alisema, "Nanyi mtafanya zaidi ya hili." Unaona, alilithibitisha Andiko Lake kuwa sahihi! Tembeeni kuingia ndani sasa. Hebu sote tuombe sasa kwa ajili ya hawa watu walioko hapa. Kila mtu anayejua jinsi ya kuomba. Ni Wakristo wangapi waliozaliwa upya walioko ndani ya jengo? Inua juu mkono wako. Sasa hebu kila mmoja tuinue juu mikono yetu na kutoa shukrani kwa ajili ya hawa watu.

96 Baba yetu wa Mbinguni, tunatoa shukrani Kwako kwa ajili ya hawa watu. Wao ni wa Kwako. Wamekuja, na wanaungama. Wamekuja na kufa nafsi na dhambi. Wao wanarejea, viumbe vipya katika Kristo.

Shetani, umeshindwa vita! Mungu ni Yehova-Yire! Bwana amejipatia Dhabihu, ametoa watu, ametoa wito wa madhabahu, ametoa Ujumbe, ametoa neema. Na Shetani ameshindwa vita, katika Jina la Yesu Kristo yeye ameshindwa vita!

www.messagehub.info

Mahubiri Na
William Marrion Branham
*"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7*